# Nipashe

Jumanne Aprili 28, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580217

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII



guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




TOLEO MAALUMU

## Ladislaus: Dk. Mengi alikuwa zaidi ya rafiki Under The Same Sun

UKURASA 3




UKURASA 11

# Bashungwa atangaza ukomo bei ya barakoa

UKURASA 2




Kama unajisikia kuumwa na kuhisi una dalili kwa mbali jitenge. Hata kama haujakutana na mtu mwenye Covid – 19 na unahisi una dalili za ugonjwa huo, jitenge na jiangalie mwenyewe. WHO

- Epuka mikusanyiko ya watu
- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

## Bei elekezi ya sukari yapuuzwa kila kona

UKURASA 7



## Mwili wa DC Mtwara kuzikwa na watu 10

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store



MICHEZO MIEMBENI WAITAKA ZFF KUFUTA LIGI Z'BAR UK.23

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

# Bashungwa atangaza ukomo bei ya barakoa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, amesema atachukua hatua kwa taasisi zisizo za kiserikali (NGO) zinazouza barakoa kwa gharama kubwa.

Bashungwa alitoa tahadhari hiyo mkoani Arusha, alipotembelea viwanda vya kuzalisha nguo vya Sunflug na A to Z kuangalia hali ya uzalishaji wa barakoa katika viwanda hivyo.

Bashungwa alitoa onyo kwa NGO zilizoomba kibali cha kuzalisha barakoa kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania lakini badala yake wanauza barakoa kwa Sh. 2,500 hadi 3,000.

"Wamekuwa wakitoa masharti kupitia mitandao ya kijamii kuwa hawauzi barakoa chini ya bei hiyo."

"Sitawataja kwa leo, lakini nikiona tu wanauza kwa bei kubwa sitasita kuwachukulia hatua, maana mnakuja kuomba vibali, kumbe mnafanya mtaji," alisema.

Alisisitiza kuwa barakoa zote ziuzwe kwa bei isiyozidi Sh. 1,500 badala ya bei ya sasa ilikuwa sokoni ya Sh. 2,500, ambayo Watanzania wengi inawapa changamoto ya kumudu.

Kwa upande mwingine, Bashungwa alivipongeza viwanda vya nguo vya A-Z na Sunflug kwa kuzalisha barakoa ambazo zinawasaidia Watanzania walio wengi, na amewaahidi serikali kuwapatia ushirikiano.

Aidha, alivitaka viwanda hivyo kuendelea kuzalisha kwa wingi ili wananchi wengi wa vijijini waweze kupata vifaa hivyo vya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa corona.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, aliwataka wananchi wote wa mkoa huo kuchukua tahadhari zinazotolewa na Wizara ya Afya wanapotembelea maeneo yenye mikusanyiko.

Pia, alisisitiza kuwa ni vema sasa wafanyabiashara hao wakatengeneza barakoa kwa bei nafuu ili kuwezesha wananchi kuzinunua.

Akitoa taarifa kwa Waziri, Emmanuel Mgoma, mwakilishi wa kiwanda cha Sunflug, alisema kiwanda kina uwezo wa kuzalisha barakoa 25,000 kwa siku.

Mwakilishi wa kiwanda cha A-Z, Slyvester Kazi, alisema kiwanda kina uwezo wa kuzalisha barakoa 15,000 kwa siku.



Mkuu wa wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (katikati), akikabidhi tangi la kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka kwa mkurugenzi wa halmashauri ya wilaya ya Shinyanga, Hoja Mahiba (kushoto), lililotolewa na kampuni ya uchimbaji madini ya dhahabu Barrick kupitia mgodi wake wa Buzwagi, wa kwanza kulia ni katibu tawala wa wilaya ya Shinyanga, Boniphace Chambi, **Picha na Marco Maduhu**

# Corona yatishia miradi ya maji

**Na Salome Kitomari,**

DODOMA

WIZARA ya Maji, imesema tathmini ya awali ya corona katika sekta ya maji, imebaini kuna uwezekano wa kuchelewa kukamilika kwa baadhi miradi ya maji kutokana na wadau wa nje kushindwa kusafiri.

Akiwasilisha makadirio ya wiraza hiyo kwa mwaka 2020/21 jijini Dodoma, Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, alisema miradi mingi ya maji inatekelezwa kwa ushirikiano na wadau wa nchi mbalimbali duniani.

"Matokeo ya tathmini yanaonyesha kuwa pamoja na athari zingine, kuna uwezekano wa kuchelewa kukamilika kwa baadhi ya miradi ya maji kutokana na wadau tunaoshirikiana nao kutoka nje kushindwa kusafiri kuja kusaini mikataba au kushindwa kusafirisha vifaa vya ujenzi wa miradi kutokana na janga la corona," alisema.

Aidha, alisema wizara inaendelea kufanya tathmini ya kina na itachukua hatua stahiki katika kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), takribani watu 2,989,090 wameambukizwa, watu 207,431 wamefariki katika nchi na maeneo ya utawala 185.

Nchini jumla ya watu 284 wameambukizwa kati yake 10 wamefariki dunia.

Waziri Mbarawa alisema taasisi hizo zilielekezwa kushirikiana na mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha kuwa huduma ya majisafi na vifaa vya kunawia mikono vinawekwa katika maeneo yenye mikusanyiko ya watu wengi kama masoko, vituo vya mabasi na minada.

"Katika maeneo mengi nchini maelekezo haya yalitekelezwa na wananchi wengi wamekuwa wakichukua hatua muhimu za kunawa mikono kama njia mojawapo ya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa huu," alisisitiza.


United Republic of Tanzania
Ministry of Water

Enabel
Belgian Development Agency

**CALL FOR BIDS**
**(RE-ADVERTISED)**

**REHABILITATION OF MKONGORO GRAVITY-FED WATER SUPPLY SCHEME**

The Kingdom of Belgium through Enabel and the Government of Tanzania through the Ministry of Water, are implementing a water and sanitation project in Kigoma region. This is a 5-year project which runs through June 2022 and aims to promote provision of sustainable water supply services in the region. This intervention has three key result areas namely: 1) sustainable water supply operations and maintenance, 2) water supply scheme rehabilitation and extension and 3) promotion of safe hygiene practices in domestic water management. Under the second result area, the Water and Sanitation Kigoma Region Project (WASKIRP) is now inviting bids from qualified construction companies and consulting firms for the works program for the Mkongoro Gravity-fed water supply scheme.

**Rehabilitation Works**
This public works contract will consist of construction of a new intake, a treatment plant, transmission mains and distribution network which includes distribution points, in conformity with the conditions of the provided tender documents. The preferred contractor will have demonstrated financial and technical capacity to carry out the assignment described in the specifications of this tender.

**Duration:** 8 months with a post-construction defects liability period of 12 months.
**Location:** Mkongoro in Kigoma rural district in the region of Kigoma.

**More information and bid documents of these two assignments are available at: https://btctanzania.wordpress.com/**

**The works contract notice is also published on the Enabel website, www.enabel.be, in the Belgian Public Tender bulletin (BDA) and on the Organisation for Economic Cooperation and Development (OECD) website.**

215712002


# Wasiozidi 10 kuuzika mwili wa DC Mtwara

**Na Waandishi Wetu**

UONGOZI wa Mkoa wa Mtwara, umesema mazishi ya aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Evodi Mmanda, yatafanyika Mtwara chini ya usimamizi wa serikali na kuhudhuriwa na watu wasiozidi 10.

Umesema hatua hiyo imechukuliwa kwa lengo la kuzingatia na kusimamia taratibu za Wizara ya Afya kuzuia mikusanyiko katika kipindi hiki cha mlipuko wa virusi vya corona.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, aliyasema hayo katika mkutano wake na waandishi wa habari na kueleza taratibu za mazishi ambayo hata hivyo hakutaja tarehe ya kufanyika kwake.

Alisema kutokana na taratibu za tahadhari ya corona zilizoelekezwa na Wizara ya Afya, serikali inalazimika kuzika mwili huo na mazishi yake yatahudhuriwa na watu wasiozidi 10 ili kuwa na hadhari ya maambukizo ya ugonjwa wa corona.

Alisema familia ya marehemu imetoa ushirikiano mkubwa na taratibu za kuuhifadhi mwili zinaendelea na kuwasisitiza wananchi wa Mkoa wa Mtwara kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo.

Alisema Mmanda alianza kujisikia vibaya Ijumaa akiwa ofisini na hivyo kulazimika kwenda kupata matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa (Ligula) na hali ilivyozidi kuwa mbaya, alilazimika kulazwa mpaka juzi majira ya saa tano usiku alipoaga dunia.



DK. REGINALD ABRAHAM MENGI

"Unaweza kubadilisha maisha yako endapo utakuwa na imani ya dhati ya vile unavyotaka kuwa."

# Ladislaus: Alikuwa zaidi ya rafiki Under The Same Sun

**Na Beatrice Shayo**

SHIRIKA la Under The Same Sun (UTSS) ni miongoni mwa mashirika ya makundi ya watu wenye uhitaji maalumu ambalo linakumbuka msaada mkubwa uliotolewa na Dk. Reginald Mengi, hadi lilipofikia.

Shirika hilo ambalo linahudumia watu wenye ualbino, linasema Dk. Mengi alijitoa kwa namna ya kipekee.

"Kuwa kama alivyokuwa Dk. Reginald Mengi sio kazi rahisi, inahitaji nia thabiti na ya dhati ndiyo maana mchango wake unakumbukwa kwa sababu alifanya kwa namna ya kipekee." Aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la UTSS, Berthasia Ladislaus anasema.

Anasema alitoa kipaumbele cha matangazo ya shirika hilo bure kwenye magazeti yake chini ya kampuni ya The Guardian Limited.

"Wakati Under The Same Sun ilipotangaza kutafuta watu wenye ualbino waliokuwa wanahitaji ufadhili, alitusaidia kutoa matangazo bure na watu wengi waliomba. Kati ya walioomba hadi sasa wanaendelea kunufaika. Naweza kusema alitoa mbegu nzuri kama mchango wake kusaidia watu wengi," anasema Berthasia.

Katika jamii pia alishiriki matukio mbalimbali ikiwamo mikutano ya mikusanyiko ya watu wenye ualbino na alihudhuria kama rafiki wa shirika na kutoa ujumbe mzuri wa kuhamasisha jamii.

"Aliwaeleza ulemavu sio kitu cha kushindwa kutumia fursa zako na kukua kiuchumi, wapo ambao wanaendelea kunufaika katika maisha yao na kuanza kufunguka na kuona wanathaminika katika jamii."

Anasema mchango wa Dk. Mengi unakumbukwa kwa kuwatambua na kuwapa nafasi watu wenye ualbino na wenye ulemavu mwingine.

"Kumsaidia mtu sio kwa kumpatia vitu pekee hata kuwa na muda naye, tenga muda kwa ajili ya kuwa naye, kumuonyesha upendo sio tu kutoa, Mengi utoaji wake ulikuwa unaogusa maisha ya watu, naamini watu wenye ulemavu wa ngozi, Shirika la Under The Same Sun kwa ujumla watakuwa wanamkumbuka kwa hilo na watakuwa wanaendelea kufurahia matunda yake kama upendo zaidi aliouonyesha kwao."

Berthasia kwa sasa anafanyakazi kwenye Taasisi isiyo ya kiserikali inayojishughulisha na ukaguzi wa hesabu pamoja na kuandaa hesabu za watu mbalimbali inayojulikana kama African Mark Services.



Dk. Reginald Mengi akikata keki pamoja na Afisa Mtendahi Mkuu wa Under the Same Sun, Peter Ash (wapili kushoto) aliyekuwa Mkurugenzi wa taasisi hiyo Berthasia Ladslaus (kulia) na Sevelyne Nicholous katika maadhimisho ya miaka 10 tangu kuanzaishwa kwa taasisi ya hiyo.

> Sheria inatekelezeka ingawa kuna baadhi huwa wanasema wameshindwa kutekeleza kwa madai ya kukosa wenye vigezo.



Dk. Mengi akizungumza na watu wenye ualbino katika moja ya maonyesho ya wajasiriamali kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam. **PICHA ZOTE NA MPIGAPICHA WETU**

"Nikiwa kama mtaalamu wa kuandaa na ukaguzi wa hesabu, Mengi alikuwa na mchango mzuri katika Bodi ya Taifa Wahasibu na Wakaguzi (NBAA), alipokuwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo tunamkumbuka mchango wake katika taaluma hiyo na ukaguzi, inatufundisha na inatupa ujumbe mzuri kwa sisi ambao tunafanya taaluma kama yake kuona tunaweza kuisaidia jamii kwa ukaribu zaidi."

Berthasia anakumbuka utaratibu wa Dk. Mengi wa kuandaa chakula kwa ajili ya watu wenye ulemavu na matukio hayo yameacha msingi mzuri ambao ni endelevu.

Anakumbuka pia katika kitabu alichokiandika cha 'I can, I must, I will... kwamba kadri alivyokuwa anakisoma kilikuwa kinampa kumbukumbu nzuri aliyoiacha sio kwake tu bali kwa Watanzania wote ambao watafanikiwa kukisoma kitabu hicho.

"Mimi binafsi ninamuenzi Dk. Mengi nikiwa kama Mkaguzi wa hesabu, nitatoa mchango wa mawazo kutokana na kazi ninazozifanya katika jamii inayonizunguka kuwapatia kwa mfano watu wenye ulemavu kushiriki katika kampeni, kusaidia wenye uhitaji," anasema.

"Pia tunawahamasisha watu wengine kusoma kitabu chake na kukuelewa, hii ni sehemu ya kumuenzi ili jamii iweze kujifunza yaliyo mazuri na kuyaendeleza ili kile ambacho amekifanya kisiishie pale bali kiwe endelevu kwa manufaa ya jamii," anasema.

## USHAURI

Anashauri kwa wale wenye uwezo au nafasi pamoja na majukumu yao ni muhimu kukumbuka mahitaji katika jamii na hasa wenye ulemavu.

"Kama una nafasi, uwezo katika jamii ni vizuri kutenga muda wa kutambua mahitaji ya watu na kuonyesha upendo na kujua jinsi gani ya kumsaidia, mfano kama kuna mtu anatengeneza sera anasaidia watu katika nafasi yake ni lazima atenge muda kuelewa undani wa uhitaji wa watu," anasema.

"Tusiishie tu kutoa bali tupate muda wa kutoa kwa upendo kama ilivyokuwa kwa Dk. Mengi alivyokuwa akiandaa chakula cha watu wenye ulemavu na kukaa nao pamoja na wengine kuwasikiliza shida zao."

## WENYE ULEMAVU WAKUMBUKWE AJIRA

Anasema hata sheria inaelekeza kutoa nafasi kwa aliye na ulemavu.

"Mtu aguswe kutoa ajira kwa kuwa ni jambo zuri, kama alivyokuwa anafanya Dk. Mengi kutoa kipaumbe kwa wenye ulemavu anapotoa ajira," anasema.

Anasema sheria inatekelezeka ingawa kuna baadhi huwa wanasema wameshindwa kutekeleza kwa madai ya kukosa wenye vigezo.

"Mtu akiwa na nia ya dhati hata kama amekosa wenye uwezo hakikisha anaweka nafasi ambazo zitawasaidia kuwainua hata kupitia mafunzo mbalimbali ili waweze kufikia vigezo unavyovitaka, tusitumie sheria peke yake kuwe na wigo wa kumsaidia,"anasema.

## KILICHOMGUSA

Dk. Mengi ni kusimamia majukumu yake maalum kwa wakati kama binadamu, utamkuta katika taaluma yake, biashara, yupo na watu wenye uhitaji na familia yake.

Tusiishie kujifunza, tuyaenzi nasi tufanye yaliyo mazuri zaidi," anasema.

# MUCOBA BANK PLC

P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075 ,

Mafinga, Tanzania.

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 32 kifungu namba 3 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2006**

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31/03/2020 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya/Mwaka wa sasa | Robo Mwaka/Mwaka iliopita |
|---|---|---|---|
| | | 31/03/20 | 31/12/19 |
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslim | 674 | 485 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu Ya Tanzania | 269 | 242 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio katika Benki Nyingine na Taasisis za Fedha | 1,856 | 1,539 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizo afikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizo kubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki nyingine | - | - |
| 10 | uwekezaji katika Amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 10,730 | 10,460 |
| 12 | Mali nyingine | 4,269 | 3,917 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa. | 391 | 425 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **18,189** | **17,069** |
| | | | |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisis za Fedha | 3 | 3 |
| 18 | Amana za Wateja | 15,590 | 14,588 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 95 | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Benki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 39 | 142 |
| 24 | Dhima la Tozo KWA Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi. | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 670 | 619 |
| 28 | Madeni | 2,946 | 3,045 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **19,343** | **18,397** |
| 30 | **MALI(DHIMA) HALISI (16 Kutoa 29)** | **(1,154)** | **(1,328)** |
| | | | |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 2,764 | 2,764 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (4,203) | (4,612) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 175 | 409 |
| 35 | Akaunti nyingine za Mtaji | 111 | 111 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEHDA ZA WANAHISA** | **(1,154)** | **(1,328)** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 0 | 0 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 960 | 1017 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 774 | 766 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 0 | 0 |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Amana | -6.34% | -7.78% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo ghafi | 8.35% | 9.06% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 68.82% | 71.70% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 58.99% | 61.28% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zilizozalisha na Jumla ya Mali | 69.20% | 70.30% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 6.87% | 5.61% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 6.56% | 2.94% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZ KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31/03/2020 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa | Robo ya mwaka linganishi (Mwaka uliopita) | Limbikizo lamwaka sasa | Limbikizo la mwaka linganishi (mwaka uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 31/03/2020 | 31/3/2019 | 31/03/2020 | 31/3/2019 |
| 1 | Mapato ya Riba | 831 | 803 | 831 | 803 |
| 2 | Gharama za Riba | 139 | 209 | 139 | 209 |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | 692 | 594 | 692 | 594 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 8 | 35 | 8 | 35 |
| | | | | | |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **183** | **164** | **183** | **164** |
| | 6.1 Faida/ (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | - | - | - | - |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 118 | 104 | 118 | 104 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 65 | 60 | 65 | 60 |
| 7 | **Gharma Zisizo za Riba:** | **692** | **720** | **692** | **720** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 307 | 276 | 307 | 276 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 11 | 54 | 11 | 54 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 374 | 391 | 374 | 391 |
| 8 | **Faida/ (Hasara) ya Uendeshaji** | **175** | **2** | **175** | **2** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | 1 | - | 1 |
| 10 | **Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **175** | **2** | **175** | **2** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **175** | **2** | **175** | **2** |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | 58 | 53 | 58 | 53 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 21.46 | 0.28 | 21.46 | 0.28 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na wastani wa mali | 0.99% | 0.05% | 0.99% | 0.05% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya kodi na wastani wafedha za wanahisa | -14.10% | 0.33% | -14.10% | 0.33% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya riba na mapato ghafi | 68.23% | 74.53% | 68.23% | 74.53% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 3.72% | 2.86% | 3.72% | 2.86% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa mwezi inayohusika katika kipindi na kugawanywa kwa idadi ya mwezi katika kipindi hicho**

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31/03/2020 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la zaidi ya jumla | Mengineyo Bainisha | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **2,764** | **-** | **(4,203)** | **24** | **87** | **-** | **(1,328)** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 175 | - | - | - | **175** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na Wanahisa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | **-** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **2,764** | **-** | **(4,028)** | **24** | **87** | **-** | **(1,154)** |

| | Mtaji wa hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la zaidi ya jumla | Mengineyo Bainisha | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | **2,748** | **-** | **(5,556)** | **504** | **88** | **1** | **(2,215)** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 409 | - | - | - | **409** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | **-** |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | 944 | (480) | (1) | (1) | **462** |
| Mengineyo | 16 | - | - | - | - | - | **16** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **2,764** | **-** | **(4,203)** | **24** | **87** | **(0)** | **(1,328)** |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31/03/2020 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka yasasa | Robo ya Mwaka iliyopita | Limbikizo la mwaka wa sasa | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 31/03/2020 | 31/12/2019 | 31/03/2020 | 31/12/2019 |
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uendeshaji** | | | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 175 | 211 | 175 | 2 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | Hasara Katika Mali | 42 | 57 | 42 | 21 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (270) | (1,000) | (270) | 340 |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | 1,097 | 551 | 1,097 | (1,537) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mabadiliko halisi Katika Dhima Nyingine | (52) | (327) | (52) | 462 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (352) | (531) | (352) | 484 |
| | Kodi Iliyolipwa | (9) | (8) | (9) | (8) |
| | Mengineyo (Bainisha) | - | - | - | (233) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli Zauendeshaji** | **631** | **(1,047)** | **631** | **(468)** |
| | | | | | |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | - | - | -2 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya mali zakudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya amana Zisisoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **-** | **-** | **-** | **-2** |
| | | | | | |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za kifedha** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | (99) | - | (99) | (60) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutoka na Utoaji wa mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | -1 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | 665 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa shughuli zakifedha Kifedha** | **(99)** | **-** | **(99)** | **604** |
| | | | | | |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu.** | | | | |
| | Ongezeko /Punguzo Halisi Katika | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | 532 | (1,042) | 532 | 134 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 2,266 | 3,308 | 2,266 | 2,110 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **2,799** | **2,266** | **2,799** | **2,244** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 3/31/20

Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, Sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita ( kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| *Jina Na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| **Philipo Raymond** **Meneja Mkuu** | ......................................(Imesainiwa) | **28th April, 2020** |
| **Kelvin Mushi** **Meneja wa kitengo cha Fedha and Utawala** | ...................................... (Imesainiwa) | **28th April, 2020** |
| **Hilda Valerian** **Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | ...................................... (Imesainiwa) | **28th April, 2020** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunadhibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa za uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonyesha hali halisi

| **Jina** | **Tarehe** |
|---|---|
| **1. Prof.Domicus Kasilo.............................. (Imesainiwa)** Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi | **28th April , 2020** |
| **2. Bw.Kitova Mungai ...................................... (Imesainiwa)** Mkurugenzi | **28th April , 2020** |

## MINIMUM DISCLOSURES OF CHARGES AND FEES

| SAVINGS ACCOUNT | CHARGES AND FEES |
|---|---|
| **Individual Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Credit Interest Rate | 2% |
| | |
| **Joint Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Credit Interest Rate | 2% |
| | |
| **Juvenile's/ Minor Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Biashara Savings Account** | |
| Account Opening minimum amount | 65,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 50,000 |
| Monthly Service Fee | 5,000 |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Group Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Saccos Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 55,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 100,000 |
| Monthly Service Fee | 2,000 |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Elimu Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 10,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Malengo Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 5,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | See Table below |

**Malengo account interest rates are as follows:**

| Period | | Rate |
|---|---|---|
| 3 months | | 4% |
| 6 months | | 5% |
| 12months | | 6% |

**FIXED DEPOSIT ACCOUNTS**

| Period | Range | Rate |
|---|---|---|
| 3 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 4.00% |
| 6 months | Up toTzs 9,999,999.00 | 4.50% |
| 9 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 5.00% |
| 12 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 6.00% |
| 24 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 7.00% |
| 36 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 8.00% |

FDR of Tzs **10,000,000** and above is **negotiable** at management discretion.

| GENERAL CHARGES/ FEES | TZS |
|---|---|
| | |
| **Dishonored/Unpaid cheque** | |
| Fund related | NA |
| Technical | NA |
| | |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS** | |
| Cash deposit at branch | Free |
| Cheque clearing (up to Tzs 1,500,000) | 15,000 |
| Cheque clearing (above Tzs 1,500,000) | 1% |
| Cash withdrawal- (less Tzs 5,000,000) | 1,000 |
| Cash withdrawal- (Tzs 5,000,000 and above) | Tzs 1,000 plus 0.08% of excess above 5,000,000, Max Tzs 150,000 |
| Account closure | 15,000 |
| Dormant account reactivation | 3,000 |
| Dormant account monthly Fee | 1,000 |
| Premature/cancelled Fixed Deposit Fee | No interest given |
| Interim Statement Fee | 1,000 |
| Audit confirmation Fee | 10,000 |
| Balance certificate Fee | 20,000 |
| Reference Letter | NA |
| TT Outward local-TISS | NA |
| TT Outward local- EFT | NA |
| TT Inward local- TISS | NA |
| TT Outward local- EFT | NA |
| Salary Processing (per entry) | 2,500 |
| Bank Guarantees | NA |
| Balancy Inquiry | 100 |
| Money Transfer | 12,000 |
| ATM card replacement | 15,000 |
| ATM w/drawal Fee (on us) | 1,300 |
| To other bank ATMs w/drawal Fee | 1,300 |
| ATM mini statement | |
| Wallet to Bank | 1,000 |
| SMS alart | 1,000 |
| Bank to Wallet (Below Tzs 100,000) | 1,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 100,000-199,999) | 1,300 |
| Bank to Wallet (Tzs 200,000-299,999) | 1,700 |
| Bank to Wallet (Tzs 300,000-399,999) | 2,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 400,000-499,999) | 2,500 |
| Bank to Wallet (Tzs 500,000-599,999) | 3,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 600,000-699,999) | 3,500 |
| Savings account interest rates | 2% |

## HABARI KITAIFA




Mwananchi wanaotumia barabara ya kuingia na kutoka sokoni, wakipita kwa shinda kutokana taka zilizojaa katika soko la Kawe, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# Naibu Meya Moro afariki dunia

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

BARAZA la Madiwani la Manispaa ya Morogoro, limepata pigo baada ya Naibu Meya wake, Isihaka Sengo, kufariki dunia jana.

Alikutwa na mauti wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) alipokuwa amelazwa kwa siku tatu.

Taarifa za kifo chake zilithibitishwa na Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Sheila Lukuba.

Akizungumza na waandishi wa habari, Meya wa Manispaa ya Morogoro, Paschal Kihanga, alisema, Sengo alifariki dunia alfajiri.

.Alisema kwa sasa mwili wa marehemu Sengo umehifadhiwa katika hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro.

Sengo alichaguliwa kuwa Diwani wa Kata ya Kiwanja cha Ndege Januari 24,2017, katika uchaguzi mdogo baada ya aliyekuwa diwani wa kata hiyo, Godfrey Mkondya, kufariki dunia Februari 2016, ambaye alichaguliwa katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 2015.

Julai 12, 2018 ndipo Sengo aliingia katika kinyang'anyiro cha kuwania Unaibu Meya, aliapishwa kuwa naibu meya wa Manispaa ambapo alidumu kwa vipindi viwili hadi sasa.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Morogoro, Shaka Hamdu Shaka, alisema wamepokea taarifa ya msiba huo kwa masikitiko makubwa kwa kuondokewa na diwani wao.

# Serikali yapokea bil. 15/- kuikabili corona

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imepokea msaada wa Sh. bilioni 14.9 kutoka Global Fund, Airtel Tanzania na Rotary Club Tanzania, zitakazotumika kununua vifaa kinga kwa watumishi wa afya na vifaa tiba kwa ajili ya kuwahudumia walioambukizwa virusi vya corona.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alithibitisha kupokea msaada huo jana, akipokea pia lita 1,250 za vitakasa mikono kutoka kwa wadau.

"Global Fund imetoa Sh. bilioni 14, Airtel Tanzania Sh. milioni 700 na Rotary Club Tanzania Sh. milioni 250," alisema.

Waziri Ummy alibainisha kuwa kati ya Sh. bilioni 14 zilizopokewa kutoka Global Fund, Sh. bilioni 9.6 wamezitoa kununua vifaa kinga kwa ajili ya watumishi wa afya.

"Kipaumbele chetu ni kuwalinda watumishi wa afya, ninatumia fursa hii kuwashukuru watumishi wa afya ambao wamekuwa wakijitoa usiku na mchana katika kutoa huduma kwa watu waliopata corona pamoja na wale wahisiwa," alisema.

Ummy alisema kipaumbele cha serikali ni kuwalinda watumishi wa afya kwa kununua vifaa kinga ndiyo maana fedha walizopatiwa wanazielekeza huko.

"Niendelee kuwasisitiza watumishi wa afya wazingatie miongozo ya magonjwa ya kuambukiza," alisema.

Waziri Ummy alisema watumishi wa afya ambao wamepatiwa mafunzo katika vituo vya kutoa huduma kwa wenye maambukizo ya corona hakuna aliyepata kutokana na kuzingatia miongozo ya serikali ya kutoa matibabu.

"Ninapenda kurudia tena kwa niaba, Rais John Magufuli, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ninawashukuru Airtel Tanzania, Serengenti Breweries na Rotary Club kwa hiki mlichotupatia. Asanteni sana," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Airtel Tanzania, Gabriel Malata, alisema wametoa fedha hizo ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali za kupambana na janga la corona.

"Bodi ya wakurugenzi wa Airtel na kwa niaba ya Airtel Tanzania, tunatambua juhudi za serikali katika kupambana na ugonjwa huu, tumejitathmini na kutambua hatuwezi kuendelea bila watu wanaotumia huduma zetu." alisema.

Mkurugenzi wa Uhusiano wa Kampuni ya Bia ya Serengeti, John Wanyancha, alisema kampuni hiyo imetoa lita 1,250 za vitakasa mikono vyenye thamani ya Sh. milioni 15 ili kuunga mkono serikali.

Mwenyekiti wa Rotary Club, Agnes Batenga, alisema wametoa Sh. milioni 250 kwa ajili ya kupambana corona.

"Sh. milioni 183 zitatumika kutoa msaada wa vifaa vya kujikinga (PPE), vifaa vya maji safi ambavyo vitasambazwa katika vituo maalum vya kuhudumia wagonjwa wa corona jijini Dar es Salaam, Hospitali ya Amana, Zanzibar, Hospitali ya Mawenzi na Hospitali ya Mount Meru," alisema

Pia, alisema Sh. milioni 67 wamezitoa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kudhibiti ugonjwa wa corona nchini kupitia Club za Rotary.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

**UWEKAJI WAZI DAFTARI LA AWALI LA WAPIGA KURA**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote wa Tanzania Zanzibar na Mikoa ya Katavi, Rukwa, Singida, Dodoma, Iringa, Mbeya, Songwe, Njombe, Ruvuma, Lindi, Mtwara, Morogoro, Pwani na Dar Es Salaam kuwa itaweka wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura kwa siku tatu kuanzia tarehe 02 hadi 04/05/2020, katika vituo vilivyotumika wakati wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la wapiga Kura.

wekaji Wazi huu utafanyika kwa kuzingatia tahadhari zote za afya kuhusu kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa COVID-19 unaosababishwa na Virusi vya Corona
Uwekaji Wazi utafanyika kama ifuatavyo :-

1. SIKU: Uwekaji Wazi utafanyika tarehe 02-04/04/2020
2. VITUO: Uwekaji Wazi wa Daftari la Awali la Ubpreshaji Awamu ya Kwanza utafanyika katika Vituo vyote walivyoboreshea kilichopangwa kwenye kila Kata katika Halmashauri husika.
3. MUDA: Vituo vya kufanyia marekebisho au kuweka pingamizi vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni

**Utaratibu wa Uhakiki.**
Mpiga kura anaweza kuhakiki taarifa zake kwa njia zifuatazo:-
1. Mpiga Kura mwenyewe kufika katika kituo alichojiandikisha na kuhakiki taarifa zake katika orodha itakayokuwa imebandikwa katika kituo hicho.
2. Mpiga Kura kupitia simu yake ya kiganjani kupiga namba *152*00# na kufuata maelekezo yatakayomwezesha kuhakiki taarifa zake.
3. Mpiga kura kupiga simu namba 0800112100 na kufuata maelekezo yatakayomwezesha kuhakiki taarifa zake.
4. Mpiga Kura kuhakiki taarifa zake kupitia Tovuti ya Tume, www.nec.go.tz kwa kubonyeza sehemu iliyoandikwa 'uhakiki' na kuendelea kufuata maelekezo.

**Mambo ya kuzingatia.**
1. Mtu mmoja katika familia anaweza kukagua na kuhakiki taarifa za majina ya familia nzima.
2. Iwapo mpiga Kura amehakiki taarifa zake kwa kutumia njia yoyote kati ya hizo nne na kutaka kufanya marekebisho ya taarifa zake atatakiwa kwenda katika ofisi za Kata husika na kufanya marekebisho hayo.
3. Mpiga Kura anayehitaji kumuwekea pingamizi Mpiga Kura asiye na sifa za kuwemo katika Daftari la Awali la Wapiga Kura ataenda katika Kituo kilichopangwa kwenye kila Kata katika Halmashauri husika.

Muhimu: Kumbuka kuzingatia Kanuni za Afya kwa kufuata Maelekezo utakayopewa kituoni ili kujiepusha na maambukizi ya Virusi vya Corona

Gerald G. J Mwanilwa
Kny: MKURUGENZI WA UCHAGUZI

**Tangazo Hili Limetolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi S. L. P 10932 Dar Es Salaam, Tel.+255 22 2114963-6. Nukushi: +255 22 2113382. Barua Pepe: info@nec.go.tz. Tovuti: www.nec.go.tz.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ufafanuzi wa wizara hatima ya wanafunzi uwe endelevu

**SERIKALI** imewatoa hofu wanafunzi wenye mitihani ya taifa ambao wako nyumbani kutokana na tishio la virusi vya corona, kuwa watapata muda wa kutosha kujiandaa kabla ya kuingia kwenye mitihani hiyo.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akijibu hoja za wabunge za mjadala wa makadirio ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2020/21.

Alisema kuna taarifa zinasambazwa ambazo siyo za kweli, kuwa wanafunzi wenye madarasa na vidato vyenye mitihani watafanya mitihani hiyo shule zitakapofunguliwa, jambo ambalo siyo kweli.

Kwa mujibu wa Prof. Ndalichako, Wizara hiyo inafanyia kazi mpango ambao utawezesha wanafunzi kusoma na kujifunza vyema kabla ya kufanya mitihani ya kitaifa, hivyo kuwaeleza wanafunzi kuwa wasiwe na wasiwasi.

Prof. Ndalichako alifafanua zaidi kwamba wanafanya tathmini pia kujua ni kwa kiasi gani corona imeathiri uchumi na hasa kwenye sekta ya elimu, na kwamba watachukua hatua stahiki na kila kitu kitakaa sawa.

Alisema, baada ya janga hilo kumalizika serikali itafanya utaratibu wa wanafunzi kumaliza mitaala kama ilivyopangwa na hakutakuwa na mitihani baada tu ya kufungua shule.

Tunafikiri kwamba ufafanuzi uliotolewa na Waziri prof. Ndalichako utakuwa umewapa majibu ya uhakika wanafunzi wa vidato ambavyo vinakabiliwa na mitihani ya taifa.

Tinasema hivyo kwa kuwa tangu kufungwa kwa shule na vyuo nchini kwa maelekezo ya serikali Machi 17, mwaka huu, zimekuwa zikitolewa taarifa kadhaa zisizo sahihi na nyingi zikipotosha kuhusiana na masuala kadhaa yanayohusu wanafunzi wanaokaribia kufanya mitihani.

Taarifa hizo licha ya kuwapotosha wanafunzi hao, pia zimekuwa zikiwachanganya, hivyo kushindwa kujua ukweli kuhusiana na hatima yao ya mitihani. Hata hivyo, tunawapongeza baadhi ya wabunge waliozungumzia suala hili katika michango yao kwa hotuba ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na kutolewa taarifa hiyo kutoka kwa Prof. Ndalichako.

Tunaishauri wizara hiyo iweke utaratibu wa kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusiana na masuala muhimu yanayowagusa wanafunzi wakati huu, ambao wanaendelea kukaa nyumbani ikiwa ni moja ya tahadhari dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona.

Tunashauri hivyo kutokana na uwapo wa taarifa nyingi za upotoshaji katika mitandao ya kujamii, hivyo wakati mwingine baadhi ya watu, wakiwamo wanafunzi wenyewe kuziamini.

Kimsingi, wanafunzi wengi wa shule za msingi umri wao ni mdogo, hivyo ni wepesi kudanganyika na kuamini taarifa hata kama ni za uongo na upotoshaji kutokana na umri wao kutowaruhusu kuzichuja taarifa hizo.

Pale ambapo Wizara inatoa taarifa baada ya kuona kuna jambo halijakaa sawa au kuna upotoshaji, hatua hiyo inasaidia kuwafanya wanafunzi, wazazi na umma kwa ujumla kuelewa ukweli wa mambo.

Vile vile, tunashauri wizara iendelee kuwasaidia wanafunzi katika kipindi hiki ili mbali na kuwa nyumbani, waweze kupata mahitaji muhimu ya kitaaluma. Hii ni kwa sababu wanafunzi wa vidato vya mitihani watakuwa wanaendelea kujisomea kama sehemu ya maandalizi ya mitihani hiyo.

Jambo la kutia moyo na kupongeza ni jitihada ambazo Wizara ilishafanya baada ya kufungwa kwa shule Machi 17, mwaka huu.

Baada ya shule kufungwa, serikali iliondoa ada na tozo mbalimbali kwenye maktaba zake ikiwamo wanafunzi kupata machapisho na majarida kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE).


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Fursa kujifunza kusoma , kuandika zisiwapite



Na Sabato Kasika

**ELIMU** ni kati ya vipaumbele vilivyomo kwenye Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs).Ni chachu ya mageuzi inayohimizwa katika ubora, usawa na fursa kwa raia wote kujiendeleza zaidi kiujuzi na kitaaluma.

Ndiyo maana Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO), linasisitiza kuwa elimu ni kati ya haki msingi za binadamu ambayo inastahili kila mmoja aipate.

Kutokana na umuhimu huo wa elimu, Tanzania, inachukua hatua za kuwaondolea raia wake adui ujinga kwa lengo la kuhakikisha kila mmoja anajua kusoma na kuandika.

Miongoni mwa hatua hizo ni Mpango wa Elimu ya Msingi Kwa Watoto Walioikosa (Memkwa) ambao unawawezesha watoto kupata elimu nje ya mfumo rasmi.

Mpango ulioanzishwa kwa majaribio kati ya mwaka 1999 hadi 2002 katika wilaya za Musoma, Kisarawe, Ngara, Masasi na Songea Vijijini ulionyesha mafanikio na mwaka 2003 serikali ikaanzisha madarasa ya Memkwa katika shule za msingi nchi nzima.

Elimu hiyo imegawanyika katika makundi rika mawili, kundi la kwanza hujumuisha watoto walio na umri kati ya miaka 10 hadi 13, ambao husoma kwa miaka miwili hadi minne.

Baada ya hapo wanaruhusiwa kufanya mtihani wa darasa la nne na kundi la pili ni la vijana walio na umri kati ya miaka 14 hadi 18, ambapo wanaofanya vizuri katika masomo yao huruhusiwa kujiunga katika elimu ya mfumo rasmi.

Hawa hufanya mtihani wa darasa la saba, wakifaulu huendelea na elimu ya sekondari, hali ambayo kwa namna moja au nyingine inachangia kupunguza kama siyo kumaliza kabisa uwepo wa watu wasiojua kusoma na kuandika.

Katika maadhimisho ya Siku ya Kujua Kusoma na Kuandika Duniani mwaka jana, ilibainishwa kuwa watu milioni 774 hawajui kusoma wala kuandika duniani.

Wakati kukiwa na taarifa hiyo Tanzania imekuwa ikitekeleza mipango, hatua zenye lengo la kuhakikisha wananchi wanaondokana na tatizo hilo.

Kinachopaswa kuzingatiwa, ni kila mmoja ambaye hakubahatika kupata elimu katika mfumo rasmi, kuchangamkia fursa hiyo ya Memkwa ili imsaidie kujua kusoma na kuandika.

Ikumbukwe kuwa wapo wanafunzi wa mpango huo wanaofanya vizuri katika masomo yao na kujiunga katika elimu ya mfumo rasmi na kufanya mtihani wa darasa la saba, wakifaulu huendelea na elimu ya sekondari.

Elimu ni haki ya msingi kwa kila mtoto, lakini kutokana na changamoto mbalimbali, wapo ambao hawakupata fursa ya kupata elimu ya msingi katika umri unaostahili.

Kwa kuwa elimu ni silaha muhimu kumkomboa mtoto kifikra, serikali ilianzisha Memkwa ili kila mtoto aipate, na programu hii inaweza kusaidia kumaliza umbumbumbu.

Wale ambao hawakubahatika kupata elimu katika mfumo rasmi wasisite kuchangamkia programu hiyo ambayo inaweza kutimiza ndoto zao za baadaye kupitia elimu.

Ikumbukwe katika maisha kuna changamoto nyingi ambazo zinaweza kukwamisha baadhi ya watoto wakakosa elimu, lakini wakiwa na ndoto za kufanya mambo makubwa kupitia elimu.

Inapotokea fursa kama hiyo hata kama umri wao umekuwa mkubwa, bado wana nafasi ya kujiendeleza, kwa kutambua kuwa elimu haina mwisho, bado wanaweza kurudi darasani kuanza moja.

Kupitia Memkwa wananchi wajue kuwa ni njia rahisi kufuta ujinga kwa wanafunzi walioikosa nafasi katika elimu ya mfumo rasmi ingawa baadhi walioipata wapo wasiojua kusoma na kuandika

Yawezekana wakiwapo baadhi ya watu wanaodhani kwamba programu ya Memkwa haisaidii lolote, lakini wakumbuke kuwa adui ujinga hafai katika jamii, ndiyo maana miaka ya nyuma kulikuwapo na elimu ya watu wazima.

Watu wazima walikuwa wakitoka kwenye shughuli zao za kila siku na kisha jioni wanakusanyika chini ya mti wakifundishwa kusoma na kuandika, lengo likiwa ni kufuta ujinga.

Sina uhakika kama madarasa hayo ya watu wazima kama bado yana nguvu, lakini jambo la msingi ni kutambua kuwa fursa zinapopatikana zikiwamo za Memkwa, zinatakiwa kuchangamkiwa.

RIPOTI MAALUMU

# Bei elekezi sukari yapuuzwa kila kona

**Na Waandishi Wetu**

NI mwendo wa kuruka. Ndivyo inavyoweza kuelezwa juu ya bei ya sukari maeneo mbalimbali nchini, kutokana na bidhaa hiyo kuuzwa kwa bei ya juu licha ya serikali kutoa bei ya ukomo kulingana na mahali inapopatikana.


Uchunguzi uliofanywa na timu ya Nipashe katika maeneo mbalimbali nchini, unaonyesha kuwa bei ya bihaa hiyo kwa ujazo wa kilo moja inauzwa juu tofauti na bei ya ukomo iliyotangazwa hivi karibuni na serikali.

Katika kuhakikisha wafanyabiashara hawawaumizi wananchi, serikali ilitangaza bei ya ukomo katika mikoa yote nchini kuwa ni kati ya Sh. 2,600 na sh. 3,200. Hata hivyo, wafanyabiashara karibu wote wanauza kwa bei ya juu ya ukomo iliyotangazwa.

Jijini Dar es Salaam ambako bei elekezi iliyotolewa na serikali ni Sh. 2,600 baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakiuza hadi Sh. 3,400 kwa kilo huku wakijitetea kuwa wanauza hivyo kutokana na kuadimika kwa bidhaa hiyo.

Pia wafanyabiashara wengi walihojiwa na timu ya waandishi katika mikoa mbalimbali, walisema sababu ni kununua bidhaa hiyo kwa bei kubwa, hivyo kama watafanya kulingana na bei ya kikomo watapata hasara.

Kwa mujibu wa uchunguzi wa Nipashe, bei ya sukari kwa wastani wa ujazo wa kilo moja inauzwa kati ya Sh. 3,000 na 4,000 kulingana na mkoa na upatikanaji wake.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella (kulia), akimsikiliza Mkurugenzi wa kampuni ya VH. Shah, Pravin Shah, inayosambaza sukari mikoa ya Kanda ya Ziwa, baada ya kutembelea ghala la kampuni hiyo jijini Mwanza. PICHA: MTANDAO

**TANGA KIBOKO**

Mkoani Tanga, kwa mfano, katika baadhi ya maeneo, kilo moja ya sukari inauzwa kati ya Sh. 3,800 na Sh. 4,000 wakati bei elekezi iliyotangazwa na serikali kwa mkoa huo ni Sh. 2,700.

Katika eneo la Horohoro wilayani Mkinga ambako ni mpakani mwa Tanzania na Kenya, bei ya sukari imeonekana kupaa zaidi kuliko maeneo mengine ya mkoa huo.

Wafanyabiashara wengi waliohojiwa kwa nyakati tofauti, walisema wanauza kwa bei hiyo kutokana na kununua pia kwa gharama kubwa, hivyo kuuza kwa bei ya kikomo watapata hasara.

Wakati Horohoro ikiuzwa kwa bei hiyo, Muheza, Korogwe, Lushoto na Pangani sukari inauzwa kati ya Sh. 3,200 na 3,800 huku handeni na Kilindi ikiuzwa kati ya Sh. 3,800 na Sh. 4,200.

Mkoani Simiyu, kama yalivyo maeneo mengine, wafanyabiashara wameendelea kuuza sukari kwa bei ya juu kwa kile walichodai kuwa wamekuwa wakinunua kwa bei juu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana, baadhi ya wafanyabiashara walisema sukari imepotea katika maeneo mbalimbali hali iliyowalazimu kununua kwa bei ya juu ya pia kuuza kwa bei kubwa tofauti na bei elekezi ya Sh. 2,900 kwa kilo.

Kwa mujibu wa uchunguzi uliofanyika kwenye baadhi ya maduka, wafanyabiashara hao wanauza kilo 50 kwa Sh. 75,000 tofauti na awali walipokuwa wakiuza kwa Sh. 58,000 kwa ujazo huo huku bei ya rejareja ikiwa Sh. 3,500 hadi Sh. 4,000 kwa kilo.

**SHINYANGA NOMA**

Kama ilivyo kwa mikoa wa Simiyu bei elekezi ya sukari kuwa Sh. 2,900, kwa mkoa wa Shinyana bidhaa hiyo inauzwa kwa Sh. 3,000 hadi 3,500 kwa kilo.

Mmoja wa wafanyabiashara katika soko kuu la mjini Shinyanga (jina linahifadhiwa), alisema wanauza sukari kwa bei hiyo kutokana na kununua bei ya juu kutoka kwa wafanyabiashara wakubwa. Alibainisha kuwa kilo 50 wananunua kwa Sh. 142,000 wakati zamani ilikuwa Sh. 120,000.

Mkoani Iringa, bei ya sukari imekuwa ikiuzwa kwa Sh. 3,000 hadi 3,500 tofauti na bei elekezi ya Sh. 2,900 kwa kilo moja,

Baadhi ya wananchi walisema jana kuwa maagizo ya serikali yameshindwa kutekelezwa kutokana na sukari katika eneo la Miyomboni kuuzwa kwa Sh. 3,000 wakati maeneo kama ya Mkimbizi, Isakalilo, Ilala katika mji na Ilula wilaya ya Kilolo imekuwa ikiuzwa kwa Sh. 3,300.

Johari Ally, mkazi wa Mkimbizi, alisema amenunua katika moja kati ya maduka eneo hilo kwa Sh. 3,500 juzi licha ya kwamba serikali ilitangaza kushuka kwa bei hiyo.

Naye Khamis Salehe mkazi wa Ilala mjini Iringa, alisema bei ya sukari imekuwa haieleweki kwa kuwa kila duka limekuwa likiuza kwa bei yake. Alisema wako wanaouza kwa Sh. 3,000 na wengine Sh. 3,500 kwa kilo moja na alipouliza alijibiwa kuwa sukari imekuwa ya shida kupatikana na wao wanauziwa kwa bei kubwa.

**MBEYA NAKO MOTO**

Mkoani Mbeya, katika maeneo mbalimbali, sukari inauzwa kwa Sh. 3,200 na kuendelea licha ya serikali kutoa bei elekezi ya Sh. 3,000 kwa kilo.

Hatua hiyo inatokana na baadhi ya wafanyabiashara kudai kuwa wanaipata kwa bei ya juu, hivyo kuuza kwa bei elekezi watapata hasara. Wafanyabiashara hao walidai kuwa bei ya sukari imepanda na kuwafanya kununua Sh. 60,000 kwa kilo 25,000 tofauti na bei ya awali ya Sh. 48,000.

Katika mitaa ya Jiji la Mbeya, baadhi ya wafanyabiashara wa maeneo ya Veta, Ilomba, Soweto na Kabwe, kilo moja ya sukari inauzwa Sh. 3,200 wakati katika Mamlaka ya Mji wa Mbalizi inauzwa kwa Sh. 3,000 kutokana na uwapo wa sukari kutoka Zambia ambayo huingia kwa njia za panya na kuuzwa katika maduka mengine kwa Sh. 2,500.

Mkoani Pwani, katika maeneo mbalimbali ya mji wa Kibaha, wafanyabiashara wengi wameendelea kuuza sukari kwa Sh. 3,000 hadi 3,800 tofauti na bei elekezi ya Sh. 2,700 kwa kilo moja.

**KATAVI SHIDA**

Katika Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, baadhi ya wananchi wamelalamikia kukosekana kwa mifuko ya kilo 25 kwa takribani wiki mbili sasa na kusababisha walio na mitaji midogo kushindwa kumudu bei ya kilo 50 ambayo pia imepanda.

Juma Idd, mfanyabiashara wa Soko Kuu Mpanda, alisema mfuko wa kilo 25 ambao ulikuwa mkombozi kwa wenye mitaji midogo haupatikani, hivyo wameshindwa kumudu bei ya mfuko wa kilo 50 uliopanda kutoka Sh.106,000 na 112,000 hadi Sh. 147,000.

Mfanyabiashara mwingine, Stella Deus, alisema licha ya mkoa wa Katavi kupangiwa na serikali kuuza kilo moja ya sukari kwa Sh. 3,200 wanashindwa hata kuuza kilo 10 kwa siku kutokana na wananchi wengi kuwa na kipato duni.

**DODOMA BEI JUU**

Bei ya sukari jijini Dodoma imeendelea kuwa juu hadi kufikia Sh. 4,000 wakati bei elekezo ya serikali ni Sh. 2,900.

Katika baadhi ya maduka ambayo Nipashe ilitembelea jana, wako wafanyabiashara wadogo ambao wanauza sukari kwa bei tofauti kuanzia Sh. 3,000 hadi Sh, 4,000.

Mfanyabiashara wa duka la rejareja, Veronica Mushi, alisema anauza kilo moja Sh. 4,000 kutokana na kuuziwa na mawakala wa bidhaa hiyo kwa bei ya jumla ya Sh. 3,800.

Katika wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, bei imepanda hadi Sh. 3,000 tofauti na Sh. 2,600 iliyoelekezwa na serikali.

Mkoani Morogoro, wakati serikali ikielekeza kilo moja iuzwe kwa Sh. 2,700, baadhi ya wafanyabiashara wanauza kati ya Sh. 3,200 na 3,400 kwa ujazo huo.

**WATIWA MBARONI**

JESHI la Polisi Mkoani Pwani linawashikilia wafanyabiashara saba mkoani hapa kwa tuhuma za kuuza sukari kwa bei tofauti na iliyoelekezwa na serikali.

Kamanda wa Polisi Mkoani Pwani, Wankyo Nyigesa, alibainisha hayo jana mjini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Wankyo alisema wafanyabiashara hao walikamatwa katika oparesheni iliyofanywa na jeshi hilo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa wafanyabiashara hao wanauza sukari kwa bei ya Sh. 3,500 hadi 4,000 kinyume cha bei elekezi ya Sh. 2,700.

Kamanda Wankyo aliwataja wafanyabiashara hao kuwa ni Muhidini Haji (27) aliyekutwa na kilo 460, Adinani Hassan (49) kilo 112, Kassim Haji (35) aliyekutwa na kilo350, Julitha Leonard (55) kilo 55 ambao walikuwa wakiuza Sh. 3,000 kwa kilo.

Aliwataja wengine kuwa Rachel Mkumbo (23) aliyekutwa na kilo 19 huku akiuza kilo moja kwa Sh. 3,500, Omari Ramadhani (19) kilo 40 aliyekuwa akiuza Sh. 3,600 kwa kilo na Loveness Mlingi (28) kilo moja na alikuwa akiuza kwa Sh. 3,200.

Kamanda Wankyo alisema katika oparesheni hiyo, kilo 1,037 zilikamatwa na watuhumiwa wote saba ambao ni wakazi wa Kibaha wanaendelea kushikiliwa kwa mahojiano na wanatarajiwa kuchukuliwa hatua.

Licha ya kutokutaja hatua, hivi karibuni, wakati Waziri wa kilimo, Japhet Hasunga, akitangaza bei elekezi, alisema watakaokiuka maagizo ya serikali watachukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na ama kutozwa, kufutiwa leseni za biashara au vyote kwa pamoja.

Sambamba na hilo, alitoa onyo kwa wafanyabiashara wenye mtindo huo na kuwataka kuzingatia bei elekezi na atakayekiuka hatua za kisheria zitachukuliwa.

***Imeandikwa na Elizabeth Zaya na Maulidi Mmbaga (DAR), Boniface Gideon (TANGA), Happy Severine (BARIADI), Marco Maduhu (SHINYANGA), Francis Godwin (IRINGA), Grace Mwakalinga (IRINGA), Julieth Mkireri (KIBAHA), Neema Hussein (KATAVI), Paul Mabeja (DODOMA), Shaaban Njia (KAHAMA) na Ashton Balaigwa (MOROGORO).***



Fundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Bahati Mgaya, akibadilisha bomba eneo la Mlandizi wilayani Kibaha, ili kudhibiti uvujaji uliokutwa eneo hilo. Mamlaka imeendelea kuchukua tahadhali ya kujikinga na corona kwa watumishi wake wanapotekeleza majukumu yao.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kibano wenye nyumba za kupanga chawadia

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, amesema kibano kwa wenye nyumba wanaotoza kodi ya miezi mitatu, sita hadi mwaka mmoja kwa wapangaji kimewadia.

Amesema hiyo inatokana na kufikiwa kwa hatua nzuri kwa mchakato wa utungaji wa sheria ya kuwabana ambayo tayari wadau wanamalizia kutoa maoni yao.

Dk. Mabula alisema mchakato huo wa kutoa maoni uko mbioni kumalizika na tayari wadau katika kanda tano nchini wamemaliza kutoa maoni yao.

Mabula alisema pamoja na kwamba serikali imekuwa ikitoa matamko ya onyo kuhusiana na wenye nyumba kutoza kodi kwa miezi mingi kwa mkupuo kwa wapangaji, wengi wao wamekuwa wakipuuzia kutokana na matamko hayo kukosa msukumo wa sheria.

Alisema kitendo cha wenye nyumba kutoza kodi kwa wapangaji kwa miezi mingi ni kuwaumiza na serikali haiwezi kuendelea kuona hilo likifanyika.

"Serikali ilishatoa msimamo wake na matamko kuhusiana na suala la wenye nyumba kutoza kodi kwa miezi mitatu, miezi sita hadi mwaka mmoja kwa wapangaji.

"Kwa mfano mtumishi wa umma anapokea mshahara mwisho wa mwezi, halafu unamwambia alipe kodi ya miezi mitatu, sita au mwaka, anatoa wapi?

"Hata kama ni mfanyabiashara, hawezi kupata hela yote hiyo kwa wakati mmoja. Ina maana inamlazimu atafute nyingine ya ziada, jambo ambalo siyo jema.

"Kulidhibiti hili ilikuwa tatizo kwa sababu halijatungiwa sheria. Kwa hiyo, unapotoa matamko yanakubalika, lakini yanakosa msukumo wa sheria na ndiyo maana wengi walikuwa wanakaidi," alifafanua.

Dk. Mabula alisema serikali pia inaboresha Sera ya Makazi na Sera ya Nyumba, ambazo zote zinatarajiwa kutoka kwa pamoja.

"Kwa hiyo, kwa sasa tunakwenda kuwa kamili katika udhibiti wa shughuli za upangaji na hapatakuwa tena na watu kukaidi. Walikuwa wanafanya hivyo kwa sababu walikuwa wanafahamu kwamba ni maagizo tu na hayakuwa na sheria ya kuyasimamia.

"Na sisi kama wizara, hilo tuliliona na sasa tumetunga sheria hiyo na tunakwenda kulimaliza na wakati wowote itatoka," alisema.

Aliongeza kuwa mchakato wa kukamilisha sheria hiyo ikiwamo kukusanya maoni kutoka kwa wadau unasimamiwa na Chuo cha Ardhi.




# Wamlilia JPM malipo yao Nice Catering

**Na Mwandishi Wetu**

WALIOKUWA wafanyakazi ya Kampuni ya Nice Catering wamemuomba Rais John Magufuli kuwasaidia ili wapelekewe fedha zao katika mifuko ya hifadhi ya jamii, walizokuwa wanakatwa wakati wakifanya kazi katika kampuni hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, kwa niaba ya wafanyakazi wenzake 57, Jumanne Maguzo, alisema wameamua kupeleka kilio chao kwa Rais Magufuli kutokana kuzungumshwa muda mrefu.

Alisema waliachishwa kazi mwaka jana na walipofuatilia fedha za makato ambazo zilipaswa kulipwa kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii hawajakuta kiasi chochote kilichowekwa na mwajiri wao, wakati walikuwa wanachangia na wanakatwa.

Alisema walikuwa wanakatwa asilimia 10 kwenye mishahara yao kwa mujibu wa sheria.

"Mimi nimefanya kazi miaka tisa, nimeachishwa kazi naenda kufuatilia malipo yangu ya makato ya wafanyakazi hadi leo hatujapata na tukiuliza ofisini hatupewi ushirikiano," alisema Magunzo.

Maguzo alisema wamefanya jitihada za kukutana na uongozi wa kampuni ili kupata suluhu, lakini wamegonga mwamba kwani kila wakienda ofisini wanaambiwa viongozi hawapo.

Alisema wanapotumia njia ya kupiga simu ili kupanga siku ya kukutana au kuzungumza na uongozi, wamekuwa wakinyimwa ushirikiano.

Mratibu wa wafanyakazi hao, Sospeter Mtelani, aliiomba serikali kuchukua hatua za haraka katika kutatua tatizo hilo kwani maisha yao yamekuwa magumu.

"Mimi nimeacha kazi nikiwa na cheo kikubwa cha ukurugenzi na mmiliki wa kampuni, Yona Sonelo, tulikuwa karibu sana kama rafiki, amenifanyia hivi sijui hao wengine ingekuaje. Niombe Serikali ichukulie suala hili kwa uzito kwani limetuathiri sana," alisema Mtelani.

Nipashe lilimtafuta Ofisa Rasilimali Watu wa Kampuni hiyo, Jackson Charles, ili kuelekezea suala hilo, ambaye alisema: "Mimi siyo msemaji wa kampuni, labda nikupatie msemaji ndiyo atakueleza kuhusu suala hilo."

# Waziba mitaro, maji yazingira nyumba

**Na Moshi Lusonzo**

NYUMBA mbili zimebomoka na zingine 10 zimezingirwa na maji eneo la Gongo la Mboto, mtaa wa Madafu jijini Dar es Salaam, baada ya baadhi ya watu kuziba mitaro inayopitisha maji ya mvua.

Maji hayo ambayo yamechanganyika na uchafu yanatishia afya za wakazi hao kukumbwa na magonjwa ya mlipuko.

Wakizungumza na gazeti hili, baadhi ya wakazi hao walisema mafuriko hayo yanatokana na hatua ya baadhi ya watu kuziba mitaro ya asili iliyokuwa ikipitisha maji kwa kutumia matofali.

Agnes Chakulanga, alisema mafuriko hayo yalianza mapema wiki iliyopita baada ya kutokea mzozo kuhusu uhalali wa kuwapo kwa mitaro hiyo ambayo watu waliojenga jirani hawakutaka maji yapite.

Alisema majirani hao waliamua kuiziba mitaro hiyo kwa kujenga ukuta kuzuia maji hayo, ndipo yalipoanza kuzingira nyumba za na zingine kubomoka.

"Hatujui ni kwa nini hawa watu wameamua kufanya jambo hili, miaka yote mitaro ile ipo na inachukua maji kutoka Gongo la Mboto na kuipeleka mtoni. Hapa unapotuona ndani ya nyumba kuna maji na hakuna mtu anaweza kulala au kupika," alisema Agnes.

Chrisptopher Chakulanga, aliitaka serikali kuingilia kati suala hilo kwani hali hiyo ikizidi kuendelea kuna hatari ya kuibuka kwa magonjwa ya mlipuko na kuathiri wakazi wa mtaa huo.

"Maji haya yamechanganyika na yale yanayotoka kwenye vyoo vya watu, ni hatari kwa afya yetu, naomba serikali kuingilia kati haraka ili mitaro iliyofungwa izibuliwe haraka," alisema.

Mkazi mwingine, Jairos Mganga, alisema maji hayo pamoja na kuathiri nyumba za watu, baadhi wameshindwa kwenda kanisani baada ya kujaa maji.

"Watu tunashindwa kwenda kuabudu, baada ya maji kujaa kanisani, hili sio janga la mtu mmoja ni lazima hatua zichukuliwe kuweka mtaa katika amani, vinginevyo watu watashindwa kuvumilia," alisisitiza.

Mjumbe wa eneo hilo, Monica Murengelo, alisema mafuriko hayo yameleta athari kwa kubomoa nyumba mbili na zingine kumi kuwa ndani ya maji kwa muda wa wiki sasa.

Alisema baada ya kutokea kwa hali hiyo, aliamua kutoa taarifa serikali ya mtaa, kisha Halmashauri ya Ilala ili kwenda kutatua tatizo hilo.

"Nashukuru Mwenyekiti wetu wa mtaa wa Madafu amekuwa akishirikiana nasi kutatua hili tatizo, lakini bado tunasubiri serikali ichukuea hatua za haraka kutunusu," alisema Monica.

Mmoja wa watu wanaotuhumiwa kuziba mitaro hiyo ambaye hakutaka kutaja jina lake, alisema waliamua hivyo baada ya kuona wenzake wanaziba wakidai maji hayo yana uchafu kutoka vyooni.

"Mimi niliacha maji yapite katika njia yake, lakini wenzangu wa juu waliziba na mimi nikaona nifanye hivyo ili kutoruhusu uchafu kupita karibu ya nyumba yangu," alisema.

Mwenyekiti wa mtaa wa Mwembe Madafu, Mbaraka Mohamed, alisema baada ya kutokea hali hiyo, aliwasiliana na Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala, ambaye aliwatuma wataalamu wake kwenda kuangalia hali halisi kisha kuangalia namna ya kumaliza mgogoro huo.

Alisema ana imani Mkurugenzi atatatua mgogoro huo na mifereji hiyo kuzibuliwa, lakini aliomba uamuzi huo ufanyike haraka ili kunusuru maisha ya watu wa mtaa wake.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa (kulia), akipokea maelezo kutoka kwa Emmanuel Mgoma(kushoto), mwakilishi wa kiwanda cha Sunflug, ambacho kinazalisha barakoa 25,000 kwa siku. Katikati ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo. **PICHA: WVB. PICHA**

# Mgodi wafungwa viashiria hatarishi

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MGODI mdogo wa Ntambalale namba nane, uliopo kijiji cha Wisolele, Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga, umefungwa kwa muda wa siku saba baada ya kubainika kuwapo kwa viashiria vya hatari.

Mhandisi Joseph Kumburu, Ofisa Madini mkazi wa Mkoa wa Shinyanga, aliufunga mgodi huo jana, wakati alipotembelea migodi ya Ntambalale Wisolele na Kakola namba mbili na tisa kukagua utoroshaji wa madini na uchimbaji madini salama.

Alitangaza kusimamisha shughuli za uchimbaji katika mgodi huo, kwa muda wa siku saba ili viongozi wapate muda wa kurekebisha sehemu zote hatarishi ambazo zinaweza kusababisha maafa hadi Aprili 30 wawe wamekamilisha.

Vile vile, alisema sababu ya kusitisha shughuli za uchimbaji mdogo ni kutokana na wachimbaji kusogeleana, kukosa vifaa vya kijikinga na hatari ya maambukizi ya virusi vya Corona.

Pia, alisema eneo hilo linaleseni ya mwekezaji ambaye muda wowote anaweza akajitokeza na kuwaondoa na kusababisha kuibuka kwa mgogoro ambao hauna tija, na kuwataka viongozi wa mgodi huo kumtafuta mwekezaji na kuzungumza naye ili awaruhusu kuendelea na uchimbaji.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Wisolele Gold Mining, Hamisi Mabubu, alisema kwa muda uliotolewa wa siku saba, atahakikisha anarekebisha sehemu zote zenye hatari katika mgodi huo ili kumuweka mchimbaji katika hali ya usalama wakati akiendelea na uchimbaji.

Alisema, eneo hilo walikabidhiwa na serikali ya kijiji cha Wisolele kwa barua, lakini kwasasa wameshafanya mazungumzo na mmiliki wa eneo hilo mwenye leseni ili waweze kuwapatia nafasi ya kuendelea kuchimba bila kuwapo kwa mgogoro na mwenye eneo hilo.

# Mahitaji ya viuatilifu vya korosho 2020/21 yatajwa



Habari na Augusta Njoji

BUNGE limeelezwa kuwa tani 9,889.2 za salfa ya unga na lita 99,169.5 za viuatilifu ya maji vitahitajika ili kukidhi mahitaji ya viuatilifu vya zao la korosho kwa mwaka 2020/21.

Hayo yalibainishwa bungeni jana na Wizara ya Kilimo katika majibu yake kwenye swali la Mbunge wa Nachingwea (CCM), Hassan Masala.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema kumekuwa na kero nyingi sana katika sekta ya kilimo.

"Je, ni upi Mpango wa Serikali katika usambaza pembejeo za zao la korosho kwa msimu wa mwaka 2019?" alihoji.

Katika majibu ya Wizara hiyo, ilisema serikali imeendelea kuratibu na kusimamia upatikanaji wa pembejeo katika zao hilo ili kuongeza uzalishaji na ubora wa korosho nchini.

"Katika mwaka 2019, mfumo wa upatikanaji wa pembejeo za zao la korosho ulisimamiwa na Bodi ya Korosho na udhibiti wa ubora wa viuatilifu umefanywa na taasisi ya TPRI," ilisema.

Aidha, ilisema kampuni za pembejeo pamoja na vyama vya ushirika viliagiza viuatilifu na kuvisambaza kwa wakulima baada ya kuingia mikataba na Bodi ya Korosho.

"Utaratibu huo pamoja na faida nyingine umerahisisha upatikanaji wa pembejeo kwa wakati na kwa bei nafuu ya Sh. 32,000 kwa mfuko wa kilo 50 ya salfa ya unga," ilisema.



Wizara hiyo ilifafanua kuwa, katika msimu wa 2019/20 tani 19,631 za salfa ya unga na lita 280,201 za viuatilifu vya maji zilisambazwa kwa wakulima kupita vituo vya mauzo vilivyopo katika Halmashauri mbalimbali.

Ilisema hadi mwezi Desemba 2019, kulikuwa na bakaa ya jumla ya tani 20,110.79 za salfa ya unga na lita 280,830.5 za viuatilifu vya maji.

"Bodi ya Korosho ilikusanya takwimu za mahitaji ya pembejeo kutoka Sekretarieti za Mikoa inayozalisha korosho nchini ambapo mahitaji ya Viuatilifu kwa mwaka 2020/21 yanakadiriwa kufikia tani 30,000 za Salfa ya Unga na Lita 350,000 za viuatilifu vya maji," ilisema.

Hata hivyo, ilisema kutokana na bakaa iliyopo, jumla ya tani 9,889.213 salfa ya unga na lita 99,169.5 za viuatilifu ya maji vitahitajika ili kukidhi mahitaji ya viuatilifu vya zao hilo kwa mwaka 2020/21.

Ilisisitiza serikali kupitia Bodi ya Korosho inaendelea kuratibu upatikanaji na usambazaji kwa kuongeza vituo vya usambazaji, kutoa elimu ya matumizi sahihi ya pembejeo, na kuimarisha udhibiti wa ubora kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maduka ya pembejeo.

# Tanzania yazalisha wahandisi wataalamu 25,400 tangu 1961

SERIKALI imesema tangu mwaka 1961, Tanzania imezalisha wahandisi 25,401 ambao ni wahitimu na wataalamu wa Kitanzania.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti maalum (Chadema), Ruth Mollel.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji kuanzia mwaka 1961 hadi sasa Tanzania imezalisha wahandisi wangapi katika kada mbalimbali.

"Je, kwa nini wakati wa ujenzi wa barabara kuu (Highway) kwenye miji mikubwa hayatengwi maeneo ya kufanyia biashara, je, Serikali ina mikakati gani ya kuepusha ajali zinazotokea mara kwa mara kwenye miji inayofanywa biashara pembeni mwa barabara?" alihoji.

Katika majibu ya Wizara hiyo, ilisema idadi hiyo ni kutoka katika makundi mawili ambapo kwa upande wa wahandisi wahitimu wa kitanzania ni 18,727 na wahandisi wataalamu wa kitanzania 6,674.

Aidha, ilisema katika kada hizo wahandisi wamegawanyika katika fani mbalimbali kama vile uhandisi wa ujenzi (barabara, majengo na maji) wapo 10,435, uhandisi wa umeme ni 4,164, uhandisi wa mitambo na fani zinazoelekeana ni 3,882.



Wengine ni uhandisi wa mazingira ni 1,029, uhandisi katika kilimo na umwagiliaji ni 1,085, uhandisi katika mawasiliano na kompyuta ni 2,812 na uhandisi katika madini na uchimbaji wa gesi ni 1,994.

Hata hivyo, ilisema kwa kuzingatia Sheria ya Barabara ya Mwaka 2007, Kanuni na Miongozo yake eneo la hifadhi ya barabara lina jumla ya upana wa mita 60.

"Eneo hili limetengwa kwa ajili ya barabara na samani zake tu.Halihusishi maeneo ya kufanyia biashara, ujenzi wa Barabara Kuu (Highway) kwenye miji mikubwa huhusisha njia za watembea kwa miguu, waendesha baisikeli na vituo vya mabasi,"ilisema.

Vile vile, ilisema kulingana na mwongozo, hifadhi ya barabara hutengwa kwa ajili ya kuweka huduma za kijamii zikiwemo maji, simu, gesi na mikongo ya mawasiliano.

Ilibainisha kuwa haijapewa jukumu la kutenga maeneo yakufanyia biashara katika eneo la barabara na kwamba ni jukumu la Halmashauri za Miji na Majiji.

"Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) imechukua hatua mbalimbali za kuizuia ajali zinazoweza kutokea pembezoni mwa Barabara Kuu ambako kuna wafanyabiashara ndogo ndogo," ilisema.

Ilitaja hatua hizo ni kutoa elimu na kuhamasisha umma mara kwa mara juu ya Sheria ya Barabara ya Mwaka 2007 ambayo inakataza kufanya shughuli zozote za maendeleo ndani ya hifadhi ya barabara, kujenga uzio kwenye maeneo maalum na kuweka alama na mabango makubwa yenye katazo la kufanya biashara.



## Mbunge ahoji Stamico uchimbaji chokaa Uvinza

MBUNGE wa Kasulu Mjini (CCM), Daniel Nsanzugwanko, amehoji hatua zizochukuliwa na Shirika la Madini Taifa (Stamico), kuhusu uchimbaji wa madini ya chokaa yaliyopo eneo la Uvinza na Makere mkoani Kigoma.

Akiuliza swali bungeni jana, Mbunge huyo alisema katika eneo hilo kuna uwepo mkubwa wa malighafi ya kutengeneza saruji kwa mujibu wa taarifa za kijiolojia.

"Je, ni hatua gani zinachukuliwa na Shirika letu la Stamico kuchimba madini hayo ili yanufaishe Taifa na Mkoa wa Kigoma kwa ujumla?" alihoji.

Katika majibu yaliyotolewa na Wizara ya Madini, ilisema Mkoa huo una maeneo mengi yenye viashiria vya uwapo wa madini ya chokaa ikiwemo Uvinza, Makere, Nyamori, Ulombola, Milima ya Nyakachaka, Lugufu na Mto Mugundozi (Mkondossi).

"Kawaida madini ya chokaa yanayofaa kwa ajili ya viwanda vya saruji ni yale yenye ubora angalau kuanzia asilimia 48 ya Calcium Oxide (CaO - lime) na kiwango cha Magnesium oxide (MgO) kisizidi asilimia 5 kwenye miamba ya chokaa," ilisema.

Aidha, ilisema miamba inayopatikana katika maeneo ya ukanda wa magharibi ya nchi kwa sehemu kubwa ina Calcium Oxide chini ya asilimia 48 na kulingana na taarifa zilizopo, maeneo ya Makere na Uvinza yana chokaa yenye Calcium Oxide (CaO) asilimia 30 -35 na Magnesium Oxide (MgO) asilimia 16.

"Hivyo, kutokana na uwapo wa asilimia hizo kwenye mashapo ya chokaa inasababisha gharama za uzalishaji wa saruji kuwa wa juu ukilinganisha na saruji ya maeneo ya ukanda wa Pwani," ilisema.

Hata hivyo, ilisema Tanzania chokaa ambayo ina ubora mkubwa na haina uchafu na ni inayopatikana katika maeneo ya ukanda wa Pwani ambayo kwa sehemu kubwa ina ubora wa kati ya asilimia 48 hadi 56 ambacho ni kiwango cha juu sana katika ubora wa madini ya chokaa.

"Stamico itaandaa mafunzo ya namna ya wachimbaji na wajasiriamali wa Uvinza na Makere wanavyoweza kutumia teknolojia rahisi ili kuzalisha malighafi ya chokaa kwa wingi na kwa ajili ya matumizi mengine ikiwa ni pamoja na viwanda vya mbolea, mitambo ya kuchenjua dhahabu, viwanda vya ujenzi na rangi, viwanda vya chuma, dawa, vipodozi na utunzaji wa mazingira kwa kutibu majitaka," ilisema.

Nipashe
TESA
Jumanne Aprili 28, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 13

## Liwale waambiwa baada ya corona ni kupimwa mimba



Ukurasa 12

## Fursa ya kubadili chaguo itimize ndoto za wasomi



Ukurasa 14

## Corona ilivyosheheni mzigo wa athari kwa wanajamii

### OMBENI SANGA;

# Mwarobaini corona, abuni kufundisha bila mwalimu

MACHI 17, 2020 serikali ilitangaza kufunga shule zote kuanzia chekechea, msingi hadi vyuo vya kati na vikuu baada ya kubainika kwa mgonjwa wa virusi vya corona ikiwa ni hatua za kuepusha maambukizo zaidi hasa kupitia mikusanyiko kwenye maeneo ya kujifunza na kufundishwa.

Zilifungwa mwezi mmoja na zilitegemewa kufunguliwa Ijuma iliyopita Aprili 17, lakini muda umeongezwa zaidi na haijafahamika zitaendelea kufungwa hadi lini. Hali hiyo inawalazimisha wazazi, walezi, serikali na wanafunzi wenyewe kuanza kufikiria namna ya kusoma ili kufidia muda uliopotea.

Wakati wadau hao wakiendelea kutafakari hatima ya elimu kwa kipindi hiki cha maambukizo ya corona, kijana Ombeni Sanga, mjasiriamali na mbunifu hajalala. Amekuwa kazini mchana na usiku kusaidia wenzake wasioweza kujisomea wasikwame.

Sanga amevumbua kifaa kinachoweza kusambaza elimu mahali au eneo lolote lisilo na walimu, zikiwamo shule za vijijini ambako hakuna umeme wala walimu wa kutosha na hata huduma za intaneti.

Ni kwa mujibu wa taarifa inayotangazwa na Radio ya Umoja wa Mataifa Aprili 2020. Ombeni Sanga, mvumbuzi ambaye ametengeneza kifaa chenye uwezo wa kusambaza elimu katika mazingira ambayo hakuna mwalimu, analenga zaidi wanafunzi katika kipindi hiki ambacho shule zimefungwa kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa COVID 19.

Radio hiyo inamkariri akieleza kuwa kwa miaka kadhaa amekuwa akijihusisha na ufundi wa vifaa mbalimbali vya kielektroniki kabla ya kupata wazo la kuunda kifaa hiki ambacho anasema kinaweza kuwa na sauti za walimu wengi kwa wakati mmoja, akisema wanaweza hata kuwa walimu 50 wakifundisha mada au vipindi mbalimbali kwa wakati tofauti.



Ombeni Sanga, mgunduzi wa kifaa cha kufundishia kwa kurekodi sauti. **PICHA: UN NEWS**



Uboreshaji wa teknolojia ya kunawa mikono, ambayo watumiaji wanakanyaga pedeli kusukuma maji na sabuni, ni ugunduzi unaofanyika wakati huu wa kukabiliana na corona. **PICHA: MTANDAO.**

Ombeni anaeleza kuwa anaanza kwa kuandaa taarifa za vipindi na masomo mbalimbali kutoka vyanzo kadha wa kadha vinavyoandaliwa na walimu kisha anarekodi sauti za walimu wakifundisha mada za msingi za masomo kabla ya kuingiza sauti hizo katika kifaa chake kinachosambaza elimu.

Anasema anachagua kozi mbalimbali na anawarekodi walimu wanaoandaa masomo kwa utaratibu maalumu ili kuwapa nafasi za kusikika.

Swali analoulizwa ni hili anapata wapi vifaa hivyo? Kijana huyu mbunifu anasema changamoto aliyonayo kwa sasa ni kuwa ili kuzalisha kwa wingi kifaa hiki kinachotumia betri za kawaida na kisichohitaji intaneti, atalazimika kwenda kiwandani kununua vifaa vya kielektroniki vinavyowezesha kurekodi na kunasa sauti lakini uwezo huo hana kwa sasa. Ombeni ananukuliwa akisema kuwa anahitaji vitu kama 'microphone', 'capacitor' na nyaya lakini tatizo ni kuwa si wakati wote ana fedha na kifaa hicho kinauzwa.

Anasema kuwa akishaandaa kifaa hicho kuna maelekezo ya namna ya kukitumia ili kusikia sauti za walimu mbalimbali wanaofundisha masomo tofauti.

Ili Ombeni Sanga afanikiwe kufikisha huduma yake kwa watoto wa Tanzania, ni vyema taasisi zinazoshughulikia wabunifu na wagunduzi zikamtizama mbunifu huyu kwa jicho la kumsaidia ili kuwafikia wanafunzi wengi zaidi bara na visiwani.

Taasisi hizo ni kama Tume ya Sayansi na Teknolojia (Costec), Shirika la KuendelezaViwanda Vidogo (Sido) na Taasisi za Ufundi.

Hatua zilizochukuliwa na Tanzania kuepusha maambukizo zaidi zilikuwa ni pamoja na kufungwa kwa shule zote za awali za msingi hadi sekondari pamoja na vyuo vikuu kwa siku 30 kuanzia Machi 17, 2020.

Tangazo hilo lilipotolewa Dar es salaam na Waziri Mkuu , Kassim Majaliwa akisema, "Mikusanyiko yote mikubwa ya ndani na nje isiyo ya lazima imesitishwa kuanzia sasa ikiwamo shughuli za michezo, semina, matamasha ya muziki, mikutano mbalimbali kama shughuli za kisiasa, mahafali za shule na shughuli nyingine za kijamii ambazo si muhimu zitafungwa kwa siku 30 kuanzia leo Machi 17, 2020."

Kadhalika Waziri Mkuu anasema kuwa, Wizara ya Elimu itafanya marekebisho ya ratiba ya kidato cha sita ambao wanafunzi wake walitarajiwa kufanya mitihani Mei 4 mwaka huu.

Baada ya tangazo hilo baadhi ya taasisi zikaanza kutoa taarifa za wanafunzi wake watasoma na kufundishwa kupitia mitandao hasa wale waliokuwa wanasoma katika shule binafsi na katika vyuo vikuu vya nje.


Hadi sasa jitihada mbalimbali zinafanywa ili wanafunzi wasome na kwamba baadhi ya wadau wa elimu wanaliona suala hilo hasa la kusoma kwa njia ya mtandao kuwa ni gumu kwa sababu hakuna vitini vilivyoandaliwa kwa ajili ya kuwafundisha wanafunzi hao.

Pengine pia hakuna mtaala unaoweza kutumiwa kwa dharura kujifunza kwa njia ya mtandao jambo ambalo nalo linaoongeza ugumu wa kufanikisha program hiyo ya kujifunza .

Hata hivyo serikali imeanza kufundisha wanafunzi kwa redio na televisheni ili wafuatilie vipindi wakiwa nyumbani. Changamoto inakuwa kubwa vijijini ambako hakuna kompyuta, umeme, redio , betri wala simu janja za kuwafikia walimu na wanafunzi wanaohitaji kufunzwa na kujifunza.

Ndiyo maana wabunifu kama Ombeni Sanga wangehitaji kupewa msukumo mpya na msaada wa haraka ili kufanikisha kazi ya kufunza na ujifunzaji ambayo watoto wengi wanaikosa.

ELIMU
NA REUBENI LUMBAGALA



Mwanafunzi anayesoma kozi ya kemia akifanya majaribio ya kuchunguza kemikali mbalimbali kwenye maabara . Suala la kuangalia 'kombinesheni' wanafunzi wanazozipenda limeboreshwa. **PICHA: MTANDAO**

# Fursa kubadili machaguo itimize ndoto za wasomi

MUDA wa wanafunzi wahitimu wa kidato cha nne mwaka 2019 kutumia fursa ya kutimiza ndoto zao kwa kusoma tahasusi (combination), na kozi wanazozipenda umekwisha.

Wasomi hawa walipewa muda wa kubadili machaguo yao kwenye shule na vyuo mbalimbali kulingana na ufaulu walioupata kwenye mtihani wa taifa wa kidato cha nne (CSEE).

Hatua hiyo, inakuja baada ya kuwapo wa utaratibu wa kubadili machaguo ya tahasusi, shule, kozi na vyuo. Kazi hiyo ya kubadili machaguo ya tahasusi , shule au kozi za vyuo vya elimu ya ufundi ilifunguliwa rasmi Machi 25 na ilitarajiwa kuhitimishwa Aprili 19, 2020.

Uwapo wa utaratibu huu ni jitihada za Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) kuhakikisha kila mwanafunzi mwenye sifa ya kujiunga na shule au chuo, anapata nafasi hiyo kwa kutoa nafasi ya pili ya kuchagua vipaumbele vyake apendavyo.

Awali, utaratibu huu haukuwapo na ulisababisha wanafunzi wengi kukosa nafasi ya kuendelea na masomo kwani wanafunzi walikuwa wakijaza fomu za kujiunga na kidato cha tano na vyuo mara tu wamalizapo mitihani yao ya taifa ya kidato cha nne, kwa mantiki hii, walikuwa wakijaza kabla matokeo yao hayajatangazwa na Baraza la Mitihani la Taifa (Necta).

> Kuepusha hili, ndiyo maana fursa imetolewa kwa wanafunzi kujaza kwa mara nyingine taarifa zao ili kupata kile wapendacho kinachowiana na ndoto na malengo yao.

Wanafunzi walikuwa wakijaza fomu bila kuwa na ujasiri wa kutosha kwa tahasusi na kozi za vyuo kutokana na ukweli kuwa kufanya mtihani ni jambo moja na matokeo ni suala jingine.

Halikadhalika, baadhi ya wanafunzi walikuwa wakijaza tahasusi na kozi za vyuo pasipo kuwa na uelewa wa kutosha kwani zoezi hilo lilikuwa linafanyika kwa haraka baada ya kumaliza mitihani yao.

Kwa utaratibu wa sasa wa kumpa mwanafunzi fursa ya kubadili tahasusi, shule na kozi za vyuo unampa mwanafunzi uhakika wa kupata nafasi inayolingana na ufaulu wake na hivyo kutimiza ndoto za mwanafunzi za kusonga mbele kimasomo. Waziri wa Ofisi ya Rais, Tamisemi Suleimani Jafo, akielezea suala hili alisema kabla ya uamuzi huo wanafunzi wengi wamekuwa wakikosa nafasi za masomo kwa sababu tu tahasusi au kozi walizochagua kabla ya matokeo zote zimekataa hivyo utaratibu huu mpya unatoa fursa sawa kwa wote na kuondoa malalamiko.

Kimsingi, kwa utaratibu huu, mwanafunzi anapata fursa ya kusoma tahasusi, shule na kozi inayoendana na ufaulu wake. Anapofanya usajili kwa mara nyingine kwa njia ya mtandao anakutaka na tahasusi, shule na kozi ambazo zinalandana na ufaulu wake.

Hii inampa mwanafunzi uhakika wa kupata nafasi ya kuendelea na masomo. Kwa mwanafunzi ambaye ufaulu wake uko chini, hatakutana na machaguo ya tahasusi wala kozi za vyuo atakapoingiza taarifa zake mtandaoni, hivyo mwanafunzi ataelewa moja kwa moja kuwa hana sifa, na hii inampa wasaa mwanafunzi kuangalia namna nyingine ya kuweza kusoma au kufanya shughuli nyingine za kiuchumi kwa ajili ya kuendeleza maisha yake.

Kwa muda huu uliobakia, wanafunzi anaweza kujaza tahasusi kwa ujasiri mkubwa kwa kuwa anajaza huku akiwa na matokeo yake mkononi. Hii inampa mwanafunzi uhakika wa kuchagua kilicho bora kwake na ambacho kina mwelekeo mzuri kwake kitaaluma na kimaisha baadaye.

Aidha, kwa mfumo huu, mwanafunzi hawezi kuchagua tahasusi au kozi ambazo hazilandani na ufaulu wake. Mathalani, mwanafunzi aliyesoma masomo saba ya mchepuo wa sanaa, hawezi kuchagua vyuo vya ufundi kwa kuwa hakusoma masomo ya sayansi kama fizikia na kemia.

Hivyo, mfumo umeweka utaratibu mzuri kwa wanafunzi kuchagua yale tu ya yanayokidhi vigezo kulingana na masomo na ufaulu wake kwa ujumla.

Mwanafunzi anayo nafasi kubwa ya kusoma tahasusi au kozi aipendayo kama ataamua kufanya maboresho ya taarifa zake kwenye mtandao kama wizara ilivyoelekeza. Kuiacha fursa hii ipite, kunaweza kuleta athari kwa mwanafunzi kushindwa kutimiza ndoto zake kwa kushindwa kusoma apendacho kama ujazaji wake wa awali haulandani na matokeo yake aliyoyapata.

Pasipo kubadili taarifa zake mtandaoni, wizara itamuamulia cha kusoma ambapo kinaweza kuwa tofauti na matakwa ya mwanafunzi. Kuepusha hili, ndiyo maana fursa imetolewa kwa wanafunzi kujaza kwa mara nyingine taarifa zao ili kupata kile wapendacho kinachowiana na ndoto na malengo yao.

Kubadili kozi kumefungwa rasmi, hivyo, wahitimu wa kidato cha nne wanapaswa kujihakikishia kuwa usajili huo walioutamani ndiyo wanaoupata na ndiyo fursa ya kuendelea na masomo.

Wanafunzi sasa wanaelewa kuwa waliweza kubadilisha tahasusi, shule na kozi kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya: selform.tamisemi.go.tz.

Baada ya mwanafunzi kujaza taarifa zake, zitawafikishwa Ofisi za Tamisemi na watazishughulikia katika kuhakikisha kila aliyeomba anatimiza ndoto zake za kuendelea na masomo ili kuja kutumia maarifa, ujuzi na stadi alizozipata kwenye taasisi mbalimbali za elimu kwa maslahi ya taifa.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***
***Maoni: 0764 -666349.***

ELIMU

## NA SABATO KASIKA

# Liwale waambiwa baada ya corona ni kupimwa mimba

SASA ni wazi kwamba mabinti wa shule zote 17 za sekondari wilayani Liwale mkoani Lindi, watapimwa mimba watakapomaliza likizo ya kuzuia kusambaa virusi vya corona.

Kabla ya kufanyika uamuzi huo, wanafunzi 13 walikutwa na mimba katika upimaji uliofanyika kuanzia Januari, mwaka huu mara tu waliporudi shuleni baada ya kumaliza likizo ya Desemba mwaka jana.

Katika mazungumzo yake na gazeti hilo, Mkuu wa wilaya hiyo, Sarah Chiwamba, anasema wanafunzi walitokana na mimba hizo nyumbani kwao walipokuwa likizo ya Desemba na kwamba baadhi ya shule ambazo wanafunzi walipimwa na kukutwa na ujauzito kuwa ni Rashid Mfaume Kawawa, Lawale Day, Barikiwa, Mihumo na Kiangara.

"Sasa wapo likizo ambayo bado hatujajua itaisha lini, na kwa sababu mimba walizokutwa nazo walitoka nazo kwao, watakaporudi shule itabidi kazi ya kuwapima wote ianze upya," anasema Chiwamba.

Anasema, ni jukumu la wazazi na walezi kuhakikisha watoto wao wanakuwa salama wakati wote wa likizo, kwa sababu wako mikononi mwao, na kwamba wakizembea, watasababisha kuendelea kuwapo mimba.

"Lakini pia sisi tutalazimika kuwapima upya, kwa sababu wale waliokutwa na mimba walipata wakiwa likizo, hivyo huenda likizo hii nayo wakapatikana wengine wenye mimba," anasema.

Anasema, wao kama serikali wanalazimika kufanya hivyo ili kujiridhisha kama wanafunzi walikuwa salama huko nyumbani kwao, na kusisitiza kuwa kila mzazi na mlezi awe makini na mtoto wake.



Moja ya mahafali ya kidato cha nne ya Liwale High School. **PICHA: MTANDAO**

### VYANZO VYA MIMBA

Mmoja wa wakazi wa Liwale, Bakari Chikojo anasema, kuna sababu mbalimbali zinazochangia kuwapo kwa mimba na hata ndoa za utotoni, mojawapo ikiwa kiwango kidogo cha elimu ya afya ya uzazi na wazazi.

Anasema baadhi ya wazazi hawazungumzi na watoto wao kuhusu masuala ya uzazi na kwamba mtoto anapoanza kupata mabadiliko ya mwili, hivyo wazazi wanatakiwa kuzungumza naye.

"Vilevile kuna suala la umasIkini, tamaa, kufanya ngono zembe, shinikizo rika na mambo ya mila na desturi, vyote hivyo na mengine mengi ni miongoni mwa sababu za kuwapo mimba hizo," anasema Chikojo.

Anasema, amewahi kufanya kazi katika asasi moja ya kiraia inayojishughulisha na mambo ya malezi, hivyo anataja sababu ambazo ana uhakika nazo kuwa zinachangia baadhi ya wanafunzi kupata mimba.

> " Lakini pia sisi tutalazimika kuwapima upya, kwa sababu wale waliokutwa na mimba walipata wakiwa likizo, hivyo huenda likizo hii nayo wakapatikana wengine wenye mimba.



Mkuu wa Wilaya ya Liwale, Sarah Chiwamba.

"Mambo ya unyago hayana ubaya, lakini nayo yanachangia kuwapo kwa mimba, kwani watoto wa kike wanayofundishwa unyagoji, baadhi yao huyafanyia majaribio na kujikuta wanapata mimba," anasema.

Naye mkazi mwingine wa Liwale, aliyejitambulisha kwa jina la Fatma Machongwe, anasema, wazazi na walezi wakisimamia nafasi zao vizuri, wanaweza kuwa na mchango mkubwa wa kupunguza mimba hizo.

"Wapo baadhi ya wazazi wanachukulia mimba za wanafunzi au ndoa za utotoni kama jambo la kawaida na kumbe ni tatizo, ambalo wanatakiwa kusaidia kulipiga vita," anasema Fatma.

Fatma anasema, taifa linapoteza nguvukazi yake ya baadaye kutokana na wanafunzi kupata ujauzito na kuacha shule, hali ambayo ni sawa na kukatisha malengo yao waliojiwekea. Anamtaka kila mzazi au mlezi kusimama kwenye nafasi yake kuhakikisha mtoto wa kike hakutani na kikwazo chochote ambacho kinaweza kukatisha malengo yake ya baadaye kwenye elimu.

### MIKAKATI KUDHIBITI

Mkuu wa Wilaya, Sarah Chiwamba anasema, katika jitihada za kukabiliana na tatizo la mimba na ndoa za utotoni, wana mkakati wa kuanzisha klabu za wanafunzi kila shule zitakazosaidia kutoa elimu ya uzazi na mambo mengine muhimu.

Anasema, klabu hizo za kuwakutanisha wanafunzi wa kike na wa kiume ni za muhimu kwa vile zinaweza kuwa na mchango mkubwa wa kuwaweka vijana hao sawa pale wanapokutana kubadilishana mawazo.

Mkuu huyo wa wilaya anasema, kwa kukutana kwao na kujadiliana mambo mbalimbali yanayohusu masomo na hata makuzi, kunaweza kuwatoa kwenye mawazo ya kufikiria mambo ya uhusiano wa kimapenzi.

"Ninasema hivyo kwani hatua hii inaambatana na kutoa elimu ya uzazi na masuala mengine ili kumsaidia mtoto wa kike kujiamini kama njia mojawapo ya kumaliza matatizo yakiwamo ya ukatili wa kijinsia," anasema.

Anasema, kwa kutambua tatizo hilo, serikali wilayani Liwale pia inashirikiana na mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali kuendelea kufanya jitihadi za dhati za kuhakikisha inatokomeza tatizo hilo.

"Tumeanzisha pia mikakati mbalimbali ya utoaji elimu kwa jamii ya Liwale hasa wazazi juu ya madhara ya ndoa za utotoni kwa mtoto wa kike na umuhimu na haki ya mtoto wa kike ya kusoma," anasema.

Anasema, jamii inatakiwa imthamini mtoto wa kike na kulinda afya yake kwa kumuepusha na mimba na hata ndoa za utotoni ili aweze kusoma bila kikwazo chochote njiani.

### MADHARA

Anasema, yeye siyo mtaalamu wa afya, lakini anafafanua kuwa kuna ushahidi wa kutosha wa kisayansi kwamba mimba na ndoa katika umri mdogo kwa msichana chini ya umri wa miaka 18, ni hatari kiafya.

"Chini ya umri huo, mtoto bado hajawa tayari kuyakabili majukumu ya uzazi na unyumba, hivyo ni mateso tu kwake, ndiyo maana mimba hizi na ndoa vinapigwa vita kila kona nchini," anasema.

Anasema, kwa hali yoyote, kuna haja ya kukomesha tatizo hilo la mimba na ndoa za utotoni ili kuwalinda watoto wa kike, kwa vile mimba pia ni kinyume na haki za binadamu.

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Corona ilivyosheheni mzigo wa athari kwa wanajamii



Kazi za nyumbani ikiwamo kuteka maji, kufuga na kulima hasa vijijini ni shughuli wanazofanya watoto wakati huu wa likizo ya kukabiliana na corona. **PICHA: MTANDAO**

KUNA hatari ya kupoteza mwaka mmoja katika utaratibu wa elimu kutokana na kuendelea kushamiri kwa homa ya corona, hivyo kulazimisha shule na vyuo kuendelea kufungwa.

Wakati shule zilipofungwa kwa mwezi mmoja kuwezesha serikali kuchukua hatua kadhaa kupambana na kuenea kwa janga hilo, hasa kutokana na kilichotokea nchi za mbali kimsingi wanafunzi walikuwa kama wamepata likizo ya ziada.

Ila kwa muda wote wa ziada ambako likizo hiyo inaendelea, na kulingana na kinachotokea katika familia za watu, zipo athari halisi zinazotarajiwa kuonekana.

Maisha ya kuwa mwanafunzi kama zilivyo shughuli nyingine kijamii au kifamilia yana maeneo mawili, moja ni matazamio, ambayo hasa ndiyo yanatoa changamoto na hamasa ya kuendelea na maisha hayo, licha ya kuwa na sulubu za hapa na pale.

Upande mwingine ni kuvumilia, kuwa bado wakati mfupi tatizo hilo linakwisha na mtu anaanza maisha mapya, awe ni mzazi ambaye mwanae yuko shuleni, au kijana asiye na furaha eneo anapokaa na kusoma, anavumilia tu hali hiyo iishe ili asilete ugomvi endapo ataacha shule mapema. Livu ikiwa ndefu mno, 'anabanjuka.'

> Ni pale mtoto akionekana mzigo kwa sababu mzazi au mlezi amekwama ndiyo hapo athari zinaweza kutokea, kwani ni msambaratiko wa kifamilia.

Wakati kimsingi kipindi hiki cha vizuizi vya aina tofauti kutokana na corona ni mazingira ambayo kila mtu anatakiwa kuangalia yuko wapi na inabidi akutane na nani, kupungua kwa shughuli za kawaida pia kunaleta uhaba wa riziki katika maeneo mengi kwenye kijamii.

Shughuli za elimu kwa mfano zinaposimama, kuna mlolongo wa wahusika na shughuli hizo siku hadi siku ambao matazamio yao yanaathirika, kwa mfano, washona nguo za shule, wasafirishaji wawe wenye mabasi maalum au ya kawaida.

Kwa mazingira hayo, kupungua kwa vipato kutokana na vizuizi na kukwama kiasi fulani kwa shughuli tofauti kunaleta athari za utegemezi kuongezeka au kuwa hali ya kawaida kwa wale ambao walikuwa wanajimudu.

Ina maana kuwa katika familia ambayo mlezi awe baba, mama au mhusika mwingine ambaye familia hiyo inamtegea anapokuwa katika mkwamo, athari zinaanza, kila mtu anatafuta mlango wa kutokea, au njia ya kujikimu.

Ni kuingiza uwezo wa kufanya kazi katika soko ambalo tayari limedorora kwa kutokuwapo shughuli za kutosha, hivyo bidhaa ya uwezo wa kufanya kazi inakosa mnunuzi, inabaki tu hitaji la kawaida, lipangiwe pesa.

Kutokana na ulazima wa jamii kuendelea kuhakikisha huduma za aina kadhaa zinapatikana, vinginevyo hata uhai wenyewe unakuwa mashakani, mikwamo hii ya kifamilia itaathiri zaidi wanafunzi, na hasa watoto wa kike.

Pale walipokuwa wamesimama kidete kufuatia masomo yao hadi yakamilike na kutazamia labda kuendelea zaidi siku za usoni, ngoja isiyo na mwisho inabadili hali hiyo.

Walio katika familia zinazojiweza ambako hakuna manyanyaso mapya kutokana na mikwamo ya corona, ambako mtoto wa kike atajihisi anathaminiwa kama ilivyo kawaida, hapawezi kuwa na athari za wazi.

Ni pale mtoto akionekana mzigo kwa sababu mzazi au mlezi amekwama ndiyo hapo athari zinaweza kutokea, kwani ni msambaratiko wa kifamilia.

Taarifa zinazotoka nchi kadhaa ambako uzururaji wa watu nyumbani umesimamiwa kwa nguvu na vyombo vya dola kupunguza kasi ya maambukizo ya corona zinaonyesha kuwa udhaifu wa kifamilia na hata kuvunjika kwa amani kunaongezwa na hali ya kutotoka nyumbani.

Imefikia mahali ambapo Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, aliona azungumzie suala hilo mwenyewe, hali ya zuio la watu kubaki nyumbani. Imeongeza kwa kasi kubwa mifarakano.

Ni rahisi kuelewa hali hiyo kwani watu wengi wanaishi kwa kutegeana, kuondoka asubuhi na kurudi jioni au usiku kila mmoja amechoka wanalala, hakuna wakati wa mazungumzo mengi na kukumbushana machungu.

Ni katika hali hiyo ambako mwanafunzi aliyekuwa akingoja mwaka uishe aanze maisha mengine, iwe ni kwa kufaulu au kupata cheti atafute kazi, au angalau awe huru kujiamulia hali yake ya baadaye bila kubanwa na sheria, atakapoanza kuchoshwa na ngoja ya corona. Halafu haina mpaka kuwa mwezi huu au ujao au hadi Oktoba itakuwa imekwisha.

Kwa maana hiyo kuna hitilafu ya uvumilivu inayowezekana kutokea, kuwa mwanafunzi akiona shule hazifunguliwi na nyumbanii hapakaliki, siyo rahisi kuendelea kuvumilia. Ni suala la utafiti ni njia gani zinaweza kutumika kumtenganisha na nyumbani endapo anaweza akafanya vingine, ingawa hali hiyo bado haijawakuta wengi, kwani bado ni mapema tangu shule zimefunguliwa.

Kimsingi ni kuwa siyo kila mwanafunzi atarudi shuleni zikifunguliwa, na kama itapita miezi kadhaa au hata kukaribia mwaka, wengi watakuwa wamebadili mazingira, siyo lazima kuwa yatakuwa bora zaidi bali wanaweza kuwa huru zaidi, kwani la msingi katika maisha ni riziki.

Ushauri unaotolewa na wataalamu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kuhusu namna ya kukaa katika mazingira ya kizuizi, kuhakikisha afya kiakili na kimwili ni wazi unawafaa zaidi walio na mazingira bora ambayo hayategemei shughuli za kila siku kupata riziki.

Wale ambao kukaa ndani kunavuruga vipato ni kazi ngumu kubakiza akili mahali pamoja na kuelekeza mawazo katika vitu kama televisheni, vitabu au hata maombi kwani kwa Afrika suala hilo ni muhimu, ingawa ng'ambo si rahisi likatajwa au kuona limezoeleka.

Ugumu wa maisha unapunguza utashi wa kukaa pamoja, na wanafunzi bila shule unageuka kuwa mtumishi wa ndani au kuwa mzigo kwa ndugu, hivyo haitakuwa vigumu kuvumilia. Ni kukatisha masomo endapo shule hazifunguliwi mapema.

# Wanywaji pombe kienyeji waonywa corona

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

DIWANI wa Ipagala jijini Dodoma, Doto Gombo, amewaonya watumiaji wa pombe za kienyeji kuacha tabia ya kuchangia vyombo vinavyotumika kunywea ili kuepukana na virusi vya corona.

Aidha wamiliki wa vilabu vya pombe za kienyeji na wauzaji wa majumbani wametakiwa kutokuwa chanzo cha usambazaji wa virusi vya ugonjwa wa corona kwa kupuuza maelekezo kutoka wizara ya afya na viongozi wa serikali.

Diwani huyo amewataka wachukue tahadhari ya kuhakikisha wateja wao kila mmojawapo anatumia chombo chake, huku pia wakiepukana na misongamano wanapokuwa kwenye vilabu na majumbani.

Gombo alitoa tahadhali hiyo alipokuwa akitoa maelekezo kwa watendaji, wenyeviti na mabalozi wa mitaa kuhakikisha vilabu vya pombe za kienyeji na wanaouzia majumbani wanachukua tahadhari kuepukana na maambukizo ya ugonjwa huo.

Alisema katika kipindi hiki kila maeneo yanatakiwa kuchukuliwa tahadhari kubwa ya kujilinda na hakuna sababu ya kubembelezana ikiwamo kwenye vilabu vya pombe za kienyeji.

Alisema wenye vilabu hivyo wanatakiwa kuhakikisha wanakuwa na vyombo safi vinavyotumika kunywea na vinakuwa vingi na siyo vya kupokezana kwa kila mnywaji na wakifanya hivyo wanaweza kuwa chanzo cha kuenea ugonjwa huo hatari.

"Niwatake sasa hao wenye vilabu vya pombe na wale wanaouzia majumbani, wahakikishe wanakuwa na vyombo vya kutosha, na maeneo yao kuna vifaa vya kujilinda kama vile barakoa, maji na sabauni na vitakasa mikono"alisema.

Alisema hakuna sababu ya kuoneana aibu, bali kila kaya inatakiwa kutekeleza maagizo yanayotolewa na wataalamu wa afya na viongozi wa serikali.

# Askofu atia neno dawa mbadala corona

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Maombezi (EHC), Dk. Eliah Mauza, ameitaka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuhakikisha dawa zitakazotumika zinathibitishwa na mamlaka husika ili kuondoa wimbi linaloibuka hivi sasa la kila mtu kudai anayo dawa.

Kauli hiyo imetolewa muda mchache baada ya Rais John Magufuli kushauri Watanzania kutumia tiba mbadala katika kukabiliana na virusi vya corona,

Aidha Askofu huyo amempongeza Rais Magufuli kwa msimamo wake wa kutolifungia Jiji la Dar es Saalam pamoja na Watanzania kwa ujumla licha ya uwapo wa maneno ya kejeli kutoka katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

**Kila mmoja sasa anaanza kutangaza ana dawa na anaponya corona, hili suala liwekwe vizuri, Rais ametangaza kutumika kwa tiba mbadala, lakini ni vyema Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia , Wazee na Watoto isiliache jambo hili lifanywe kiholela kama ambavyo limeanza**

Akizungumza wakati akihubiri kanisani hapo, Askofu Mauza, alisema Serikali kupitia Wizara hiyo, isiruhusu suala la dawa ya kutibu corona kiholela kwani linaweza kusababisha athari kubwa zaidi kwa watu kukimbilia tiba mbadala ambayo haina uhakika.

Alisema, Wizara itumie fursa hiyo kisayansi hasa katika kukagua dawa na ili kupata zinazoweza kutumika pia Wizara iwaite wataalamu wa tiba mbadala ili waangalie kama dawa zao zinafaa.

"Kila mmoja sasa anaanza kutangaza ana dawa na anaponya corona, hili suala liwekwe vizuri, Rais ametangaza kutumika kwa tiba mbadala, lakini ni vyema Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia ,Wazee na Watoto isiliache jambo hili lifanywe kiholela kama ambavyo limeanza, dawa zithibitishwe katika maabara za kisayansi bila hivyo, Taifa litaenda pabaya," alisema.

"Nayasema haya, tukumbuke ya Mzee wa Samunge (kikombe cha babu), alipojitangaza kuwa anatibu magonjwa mbalimbali, watu wengi walikimbilia huko na wengi walikufa licha ya kunywa kikombe hicho ambacho alikuwa akitoza Sh. 500 tu, ndivyo ilivyo, watu hawatakwenda hospitali watakimbilia kwa waganga," alisema Askofu Mauza.



Raia wa kigeni wakivaa barakoa kwa ajili ya kujilinda na maambukizo ya ugonjwa wa corona, baada ya kununua kutoka kwa muuzaji katika mtaa wa CDA jijini Dodoma jana. **PICHA PETER MKWAVILA**.

# DC ajitosa utatuzi wa mgogoro ardhi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, ameutaka uongozi wa Jiji la Dodoma kufuata masharti na sheria katika kugawa viwanja vya ujenzi ili kuondoa migogoro isiyo na tija.

Kauli hiyo aliitoa mwisho wa wiki wakati alipofika kushughulikia mgogoro wa ardhi uliopo eneo la Chandulu Kata ya Tambukareli.

Katambi aliwataka uongozi huo kufuata sheria na taratibu wakati wa kugawa viwanja kwa wananchi wanaoomba kwa ajili ya ujenzi ili kupunguza migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikijitokeza mara kwa mara.

"Mfano wa mgogoro huu una muda mrefu, mahakama iliwapa haki yao ya kisheria familia hii kumiliki ardhi ya eneo lakini Jiji wameliuza kwa watu wengine, naombeni jiji kufuata taratibu na sheria katika kugawa viwanja vya ujenzi," alisema.

"Serikali imejitahidi kuondoa migogoro ya ardhi, lakini bado kuna baadhi ya viongozi wanairudisha nyuma tena kwenye migogoro hiyo, hatutakubali lazima tukemee hili," alisema.

Alibainisha kuwa tangu alipopelekewa malalamiko ya mgogoro wa ardhi alitisha nyaraka zote za ili kujiridhisha na alibaini kuwa nyaraka zinaonyesha kuwa familia ya Mohamed Omari Ibrahim inamiliki hilo tangu miaka mingi.

Aidha, aliwataka wananchi waliopewa viwanja kwenye eneo hilo kuondoka haraka kwa sababu familia hiyo ni wamiliki halali wa eneo hilo kwa sababu kuna nyaraka za mahakama zinaonyesha waliwahi kufungua kesi mwaka 2002 na mwaka 2008 walipewa haki ya kumiliki eneo hilo.

Naye Diwani wa Kata ya Tambukareli, Juma Mazengo, alisema eneo lake limekuwa na migogoro mingi ya viwanja kutokana na wananchi kuondolewa kwenye maeneo yao ya asili na Jiji kuwamilikisha wengine.

Mazengo alibainisha kuwa kwa sababu ya eneo hilo kuonekana kuwa katikati ya mji na maarufu kwa nyumba za kibiashara kuna baadhi ya matajiri wanaojitokeza kununua bila kufuata utaratibu.

Aliongeza kuwa miaka ya nyuma kuna kikundi kazi kiliundwa ili kuboresha makazi yao, lakini walishangaa uongozi wa jiji ukauza miwanja hivyo bila kuwashirikisha wenye maeneo halali.

Msemaji wa familia hiyo, Abdi Mohammedi Omari, alisema wanamiliki eneo hilo tangu mwaka 1930 na ilikuwa na ukubwa wa ekari 40, lakini wakati wa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA) ilikuja na kuwanyang'anya sehemu ya ardhi na wakabakiwa na ekari tano tu.

"Hilo tuliamua kuacha, lakini hata hili lililobaki Jiji wanataka kutunyang'anya tena?" alihoji na kuendelea:

"Tuliomba kupimiwa eneo letu lote na tulikuwa tayari kulipa gharama za upimaji, lakini hatukupata ushirikiano matokeo yake tukaambiwa kuwa eneo lilishapimwa na watu wengine wamepewa viwanja vyetu."

Aidha alisema familia hiyo walizaliwa watoto 12 lakini mmoja alifariki, waliopo hai kwa sasa ni watoto 11 ,wote wanalitegemea hilo, ila naba yao yupo ingawa mgonjwa tangu mwaka 1966 amepooza mwili wote, yupo ndani hawezi kutembea.

# Mtuhumiwa mauaji kwa kumchinja bibi mbaroni

**Na Grace Mwakalinga,**
RUNGWE

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limemkamata mtuhumiwa Hakimu Mwakifuna (20), mkazi wa Kijiji cha Nkunga, Kata ya Kiwira wilayani Rungwe kwa madai ya kumuua bibi yake, June Sankanye (55) kwa kumkata kichwa kisha kukibeba kwenye ndoo na kutokomea nacho kusikojulikana.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo juzi, Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Mbeya, Ulrich Matei, alisema Aprili 21, mtuhumiwa alifukuzwa nyumbani kwa bibi yake ambaye ni mzaa mama yake baada ya kuanza kuwatisha ndugu zake kuwa atawauwa kwa kutumia panga.

Siku mbili baadaye alienda kukaa kwa bibi yake mzaa baba ndipo alipofanya unyama huo wa kumkata na kitu chenye ncha kali shingoni na kutokomea na kichwa chake mahali kusikojulikana.

Vile vile, Kamanda Matei alikanusha uvumi kuwa mtuhumiwa huenda ana matatizo ya akili ndiyo sababu ya kufanya unyama huo na kudai kuwa suala hilo liko mikononi mwa vyombo vya sheria hivyo visiingiliwe na atapandishwa kizimbani muda wowote kujibu tuhuma hizo.

"Siamini kabisa kama huyo mtuhumiwa ni mgonjwa wa akili, maana baada ya kumbana alituonyesha wapi alikiweka na kichwa cha bibi yake na kukikuta kimeviringishwa kwenye mfuko wa sandarusi, sasa utawezaje kusema huyu mtu ana tatizo la akili," alisema Matei.

**Siamini kabisa kama huyo mtuhumiwa ni mgonjwa wa akili, maana baada ya kumbana alituonyesha wapi alikiweka na kichwa cha bibi yake na kukikuta kimeviringishwa kwenye mfuko wa sandarusi, sasa utawezaje kusema huyu mtu ana tatizo la akili**

Familia ya marehemu Sankanye ilielezea tukio hilo ambayo ilimzika marehemu bila kichwa, ilidai kulazimika kuufukua mwili na kuuzika upya baada ya kichwa chake kupatikana kikiwa kimetelekezwa ndani ya ndoo, kwenye Pagara lililopo eneo la Ilundo.

Msemaji wa familia, Harun Mwakatumbula, alisema bibi huyo aliuawa na mjukuu wake, Aprili 23, majira ya saa 11 alfajiri kwa kuchinja kichwa kwa kutumia panga.

Alisema familia kwa kushirikiana na wakazi wa Kijiji cha Nkunga, walifukua kaburi ili waunganishe kichwa na kiwiliwili na kuzika pamoja.

Alisema kichwa kilipatikana baada ya mtuhumiwa wa mauji hayo ambaye anadhaniwa kuwa na tatizo la afya ya akili kukamatwa katika eneo la Kiwira na kwenda kuonyesha sehemu alipokitelekeza.

Dada wa mtuhumiwa, Julius Mwamloka, alisema mdogo wake alikamatwa eneo la Kiwira, wakati alipoenda kwenye nyumba ya mtu mmoja kuomba maji ya kunywa, na mtu huyo alitoa taarifa baada ya habari zake kuenea maeneo yote ya kata hiyo.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Mariam Nurdin, alikiri kufukuliwa kwa kaburi la marehemu na kuzikwa upya baada ya kichwa chake kupatikana.

Alisema mtuhumiwa alikitelekeza kichwa hicho kwenye pagala, sehemu ambayo watu wanachimba mchanga, aliwashukuru wananchi wa kijiji hicho kwa ushirikiano waliotoa na kueleza kuwa ni tukio la kwanza na la aina yake kutokea eneo hilo katika kijiji chake.



Wakazi wa Kata Tembela iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wakisikiliza ushauri wa kitaalam ulitolewa na Ofisa Kilimo wa eneo hilo, Michael Boniface, juu ya faida za matumizi ya mbegu bora zinavyoongeza uzalishaji wa mazao na kumnufaisha mkulima,jana. **PICHA NA GRACE MWAKALINGA**

# RC aagiza wamiliki vyombo vya usafiri kuangalia kiwango nauli

**Na Grace Mwakalinga**, MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewataka walimiki wa vyombo vya usafiri wa umma hususani daladala kuangalia upya kiasi cha fedha wanachokihitaji kukusanya kila siku kutoka kwa madereva wao kufuatia janga la ugonjwa wa Covid-19.

Chalamila alitoa kauli hiyo, mwishoni mwa wiki wakati akiongea na madereva wa daladala wa vituo vya Kabwe na Mwanjelwa na stendi kuu vilivyopo jijini Mbeya.

Alisema kutokana na janga hilo na kutolewa miongozo mbalimbali katika kukabiliana nalo ikiwamo abiria kukaa wote kwenye siti na kupunguza msongamano imechangia malengo ya wamiliki wa daladala kutotimia ikilinganishwa na ilivyokuwa awali kabla ya ugonjwa kuingia nchini.

"Wamiliki wote wa vyombo vya usafiri wa umma hususan daladala kipindi hiki mnapaswa kuwa waungwana kwa sababu kwa hali iliyopo haturuhusu abiria kujazana kwenye magari ili kujikinga na maambukizo, msipende sana hela kuliko uhai wa Watanzania wenzetu shusheni viwango vilivyowapimia madereva wenu," alisema Chalamila.

Aliongeza kuwa madereva wa daladala wanalalamika mara kwa mara kuwa wanahatarisha kazi zao kutokana na kushindwa kutimiza malengo yao na mabosi wao wamekuwa wagumu kuelewa wakihisi wanaibiwa.

Miongoni mwa madereva hao, Justin Shaban, alieleza kuwa tangu kutolewa marufuku ya kujaza abiria ili kuzuia maambukizo ya virusi vya Corona, hali ya kiuchumi imekuwa mbaya.

Alisema awali alikuwa akipeleka malengo kwa bosi kwa siku Sh. 60,000 kwa sababu gari yake ni Coaster, lakini kwa waendesha Hiace ni Sh. 40,000.

Shaban alisema kwa sasa wanapeleka malengo kuanzia Sh. 30,000 hadi 20,000 kwa madai abiria wamepungua na katazo la kutojaza abiria.

# Kanisa lapiga marufuku watoto kuhudhuria ibada

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

MCHUNGAJI wa Kanisani la Baptist lilipo Kijiji Kibisi, Kata ya Kyimo, Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya, Oscar Katana, amepiga marufuku watoto wote kuanzia umri wa miaka mitatu hadi 15 kushiriki ibada ili kuwakinga na maambukizo ya virusi vya Corona.

Akizungumza na Nipashe jana, Mchungaji Katana alisema, walifikia uamuzi huo baada ya kubaini kuwa watoto hawana uelewa wa kujikinga na maambukizo ya virusi vya Corona hivyo njia pekee ya kuwakinga kuwazuia kushiriki ibada.

"Kanisa limepiga marufuku watoto kuanzia miaka mitatu hadi 15 kushiriki ibada kwa sababu hawezi kuchukua tahadhari yoyote kukabiliana na ugonjwa wa Covid-19 hata kama tuna ndoo za maji na vitakasa mikono, wao wataendeleza michezo na kushika vitu ovyo," alisema Mchungaji Katana.

Aliwapongeza wazazi na walezi kanisani hapo kumuunga mkono kwa marufuku hiyo wakidai tahadhari itasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza mapambano dhidi ya ugonjwa wa Covid-19.

Mchungaji Katana alitoa ushauri kwa viongozi wa dini wanapokuwa kwenye nyumba za ibada kuchukua tahadhari zote muhimu ambazo zilishauriwa na wataalam ikiwamo kukaa umbali wa kuanzia mita moja, kunawa mikono kwa maji tiririka na sababu au vitakasa kabla na baada ya ibada.

Mmoja wa waumini wa kanisa hilo, Sifa Mwanjenjele, alisema vita dhidi ya ugonjwa wa Covid-19 sio ya serikali pekee bali ni kila mwananchi katika kila eneo analotoka kwa kuhakikisha watoto wanaendelea kubaki salama dhidi ya ugonjwa huo.

## HABARI ZANZIBAR

# Balozi Iddi asisitiza umuhimu kuvaa barakoa

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema wakati umefika kwa kila mwanajamii kujenga utamaduni wakuvaa barakoa ili kujiepusha na maambukizo ya virusi vya Corona.

Alisema taifa bado liko katika kipindi kigumu kutokana na wimbi la maambukizo ya virusi hivyo ambavyo vinazunguka ndani ya mitaa baada ya serikali kufanikiwa kuzuia maambukizo kutoka nje ya nchi kwa kufuta mwingiliano wa safari za kimataifa.

Balozi Seif alitoa tahadhari hiyo mjini hapa baada ya kupokea msaada wa mashuka 20 na mashine 30 za kupimia joto la mwili zilizotolewa na mfanyabiashara Said Nasser Nassor (Bopar), akikamilisha msaada aliyoahidi katika kuungana na serikali kuu kwenye mapambano dhidi ya kuenea kwa virusi hivyo nchini.

Balozi Seif alisema ugonjwa wa mafua na homa kali ya mapafu inayosababishwa kupumua kwa shida pamoja na kikohozi umo ndani ya jamii ukisambaa jambo ambalo linahitaji kuchukuliwa kwa tahadhari kubwa.

Alisema katika vita hivyo vigumu, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inahamasisha viwanda vidogo nchini kutengeneza barakoa ili kuwapunguzia gharama kubwa wananchi hasa wa kipato cha chini wanaolazimika kununua vifaa hivyo kutoka nje ya nchi kwa bei ya juu.

Balozi Iddi alimpongeza na kumshukuru mfanyabiashara huyo kwa uzalendo wa kujitolea kusaidia jamii inapopata changamoto na mitihani tofauti.

**Alisema katika vita hivyo vigumu, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inahamasisha viwanda vidogo nchini kutengeneza barakoa ili kuwapunguzia gharama kubwa wananchi hasa wa kipato cha chini wanaolazimika kununua vifaa hivyo kutoka nje ya nchi kwa bei ya juu.**

Alisema msaada huo wa mashuka na mashine za kupimia joto la mwili zinazoashiria kuelewa kuutambua ugonjwa mapema ni muhimu na kwa upande mwingine zitasaidia nguvu ya serikali katika jitihada zake za kupambana na maradhi yanayo wasumbua wananchi.

Akikabidhi mashuka na mashine hizo za kupimia joto la mwili kukamilisha ahadi yake, mfanyabiashara huyo alisisitiza kwamba yuko tayari siku na muda wowote kusaidia jamii na serikali linapotokea suala la dharura inayoikumba jamii.

Bopar alisema hana sababu ya kutoiunga mkono serikali kuu inapotokea dharura au kuombwa kufanya hivyo kwa maslahi ya taifa na wananchi wake wote.

Wiki iliyopita mfanyabiashara huyo alikabidhi msaada wa vitanda, sabuni, vitakasa mikono, dawa ya mbu, magodoro, mito, tishu na mashuka kwaajili ya kupambana na virusi vya corona.



Mwendesha pikipiki maarufu bodaboda, akiwa abebeba nyasi huku amempakia mtu juu ya nyasi hizo, jambo ambalo ni hatari kwa usalama wao, katika eneo la Kitonga Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**.

## Zaidi ya miche 5,000 mikarafuu yatolewa bure

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

ZAIDI ya mikarafuu 5,000 imekabidhiwa kwa Masheha wa Wilaya ya Kaskazini B kwa ajili ya kuwapa wananchi waliopo katika shehia za wilaya hiyo kuendeleza kilimo hicho nchini.

Akikabidhi mikarafuu na kuzindua upandaji wa mikarafuu hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini B, Rajab Ali Rajab, alisema mikarafuu hiyo inatolewa bure kwa wananchi ili kukiendeleza na kukikuza kilimo kwa kuzalisha zao hilo kwa wingi.

Alisema kilimo hicho kina faida na wananchi wanaweza kupata kipato kitakacho wakomboa na umaskini kupitia zao hilo endapo wananchi hao watatilia mkazo kama ilivyo kwa kilimo kingine.

Alisema katika kisiwa cha Unguja, wilaya ya Kaskazini B ndiyo inayoongoza kwa uzalishaji wa karafuu na sasa mikakati yao ni kuhakikisha wanaifuatilia kwa kila mwananchi aliepatiwa ili mwakani kujua mingapi iliyoweza kukuwa vizuri.

Aliwataka Masheha kushirikiana na wataalamu wa kilimo ili kila mwananchi atakaepatiwa miche hiyo aweze kufuatiliwa na kujua maendeleo ya ukuaji wake na namna ya kuitunza.

Naye Msaidizi Mkurugenzi wa sekta ya kilimo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini B, Suleiman Khamis, alisema, matarajio yao kwa mwaka ujao ni kuzalisha zaidi ya mikarafuu 40,000 katika kitalu ili kukuza kilimo hicho ndani ya wilaya hiyo.

**katika kisiwa cha Unguja, wilaya ya Kaskazini B ndiyo inayoongoza kwa uzalishaji wa karafuu na sasa mikakati yao ni kuhakikisha wanaifuatilia kwa kila mwananchi aliepatiwa ili mwakani kujua mingapi iliyoweza kukuwa vizuri.**

# Masheha watakiwa kulinda maeneo ya bandari

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Vuai Mwinyi Mohmed, amewataka Masheha wa mkoa huo kusimamia na kulinda maeneo ya bandari hususani zile zisizo rasmi katika nyakati za jioni ili waweze kukabiliana na vitendo vya kiharifu na upitishwaji wa bidhaa za magendo katika bandari hizo zilizopo katika maeneo yao.

Alisema wapo baadhi ya wafanyabiashara wanatumia mwaya wa muda wa jioni kupitisha biashara zao hususani katika kipindi hiki cha mwezi wa Ramadhani ambao watu wengi wanakuwa majumbani kwao kwaajili ya iftari.

Aliyasema hayo kufuatia kukamatwa kwa jahazi iliyokuwa ikisafirisha sukari kutoka bandari ya mkokotoni kuelekea Tanga, Tanzania Bara, kwa njia ya magendo.

Alisema licha ya wahalifu hao kukimbia, wamefanikiwa kulipata jahazi hilo lenye jina la 'Rabi tunakuomba' likiwa na viroba 47 vya sukari vilivyokuwa vikipelekwa Tanga kupitia bandari ya Mkokotoni.

Aliwataka kulinda maeneo yote ya vivuko kutokana na baadhi ya watu kutumia bandari bubu kusafirisha vitu mbalimbali na kuisababishia serikali kukosa mapato.

Alisema ni vyema wananchi kufuata sheria kwa kuwa serikali ya mkoa itaendelea kuimarisha ulinzi katika eneo hilo na haitosita kumchukulia hatua mtu yeyote atakaekamatwa akiwa anasafirisha bidhaa yoyote kwa njia ya magendo.

Akitoa taarifa ya kukamatwa jahazi hilo, Kamanda wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) Kanda ya Kaskazini, Makame Ali Makame, alisema walikamata jahazi hilo majira ya saa 1.30 usiku katika eneo la Mkokotoni jumba la mawe wakati wakiwa katika doria zao za kawaida katika eneo hilo la bandari.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

WANAHITAJIKA FULL TIME PHARMACEUTICAL ASSISTANTS NA PHARMACY DISPENSERS. **CONTACT: 0755 903874 / 0754 275627.**


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## AMETOROKA



**RAHEL MUFURUKI MATATA,**
msichana, umri miaka 16 au 17, kabila Msubi ametoroka kutoka Buswelu, Mwanza alipokuwa akifanya kazi za ndani kama msichana wa kazi.

Anatoka kijiji cha Runazi, Kata ya Runazi, Wilaya ya Biharamulo, Mkoa wa Kagera.

**Yeyote atakaemuona atoe taarifa Polisi au apige simu namba 0757-866900 au 0789-379702**

**Taarifa ya Polisi: MW/RB/3084/2020**

157179

## KUPOTEA KWA CHETI



**Shabani Eliud Shabani anatanagza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S4335-0020 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 2014 katika Shule ya Sekondari Mgagao.**

**Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa:**
**DAR/STA/RB/261916/2020**

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA**

**SHAURI NO.07/2020**

**KENETH CHRISTOPHER MKUNDA:::::::::::MDAI**

**DHIDI YA**

**FINCA TANZANIA LIMITED..........................................MDAIWA 1**
**ISSA SALEHE BAYA.....................................................MDAIWA 2**
**VICTORIA ISSA SALEHE..............................................MDAIWA 3**

**YAH:KUITWA SHAURINI**

**KWA: 1. ISSA SALEHE BAYA**
**2. VICTORIA ISSA SALEHE**

Fahamu kwamba Keneth Christopher Mkunda amefungua shauri dhidi yenu katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 07/05/2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere mwenyekiti wa Baraza.Mnatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya tangazo hili.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Mnaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa ninyi wenyewe au wawakilishi wanaoruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka:Musipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo ninyi kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 20/04/2020.

115716902

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**
**Usimamizi wa mirathi 30/2020**

**Ombi la ROBERT BUNDALA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu FITA BUNDALA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 27/5/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 24/4/2020

Sahihi ya Hakimu

115717302

## KUPOTELEWA NA KADI YA TREKTA

**JACKSON JOSEPH SANGALA** anatangaza kupotelewa na kadi ya **TREKTA** aina ya **SWARAJ 744E** yenye namba za usajili **T 256 DRE** . Chassis **No.MBNAV53AFKCA21218** , Engine No.**433009SAA02679.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/KID/RB/274255/2020.**

115717002

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Ndugu Deus Alexander Wamala** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota Harrier yenye namba za usajili T 138 BMA, injini Na. 2AZ-FE2362 na Cheses Na. ACU10-0009542. Alidondosha bahasha iliyokuwa na kadi hiyo eneo la stand kuu ya Bukoba tarehe 01 April, 2020.

Yeyote atayeona bahasha/ kadi hiyo atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu au awasiliane naye kwa namba 0762-020849 au 0685-637016.

Ametoa taarifa polisi na kupewa RB Na. KAG/BUK/RB/329797/2020.

157185

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANDREW KUYEYANA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 529 CKM NISSAN DATSUN. Chassis namba JNIAHGD22Z0010748. Engine namba TD272664.**

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi: MWA/NY/RB/285411/2020.**

157187

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**CHINA COMMUNICATION CONSTRACTION** Inatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **Noah** yenye namba za usajili **T 141 DTB** . Chassis **No. AZR 600424033,** Engine No.**AZ 5166598.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **RB/SIM/MAS/318867.**

---

IN THE DISTRICT DELEGATE OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.18 2020
In the matter of the Estate of the LATE AZIMIO RICHARD MALAGO OF CHAN'OMBE EXTENSION AREA WITHIN DODMA REGION
And
In the matter of the Application for letters of Probate and Administration of estate by ESTHER ERNES MSOFFE

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 163)**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 29/04/2020.

Dated at Dodoma this 20th day of March 2020

PETITIONER

Presented for filling this 08/04/2020

RESIDENT MAGISTRATE


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# Watanzania wasisitizwa kumtanguliza Mungu

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, amewataka Watanzania waendelee kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa homa ya mapafu (COVID-19), huku wakimtanguliza Mungu.

"Hakuna njia nyingine yoyote isipokuwa kunyenyekea chini ya mkono wa Mungu. Tuendelee kuchukua tahadhari wakati bado tunaendelea kumtumainia Mungu. Ni heri kumwishia Mungu, na Roho Mtakatifu atatupa njia ya kutoka hapa tulipo," alisema.

Alitoa kauli hiyo juzi jioni wakati akizungumza na viongozi wa dini walioshiriki maombi maalum ya kitaifa kwa mkoa wa Dodoma dhidi ya ugonjwa wa COVID-19 yaliyofanyika kwenye ukumbi wa Chuo cha VETA, Dodoma.

Alisema Rais John Magufuli ambaye ana hofu ya Mungu na ndiyo maana aliomba Watanzania kwa imani zao wafanye maombi kwa siku tatu.

Alisema Serikali inatambua mchango wa viongozi wa kiroho na akawataka waliombee Taifa kwani mwaka huu linajiandaa kwa uchaguzi mkuu. "Mwaka huu tunatarajia kufanya uchaguzi mkuu, kwa hiyo tunaomba tumtangulize Rais wetu, tumuombee sana kwa yale anayoyafanya kwa nchi yetu."

Rais wa Chama cha Maaskofu na Wachungaji (TPA), Askofu Samson Mlawi, alitoa maombi akimuomba Mungu aifute COVID-19 kwenye mipaka ya Tanzania.

Naye mwakilishi wa Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Sheikh Kisusu Mvumbo, alisema dunia huwa inaandika historia kila kunapotokea tukio kubwa akitolea mfano wa vita kuu ya dunia. "Vita ya kwanza ya dunia iliandika historia, ikaja vita ya pili ya dunia nayo ikapita.

"Sasa hivi, tishio juu ya mdudu huyu corona pia inaendelea. Dunia haiendi imesimama, imekwama kiuchumi sababu ya mdudu corona. Tumsihi Mwenyezi Mungu atuepushe na hili janga," alisema katika maombi yake.

Mwakilishi kutoka madhehebu ya Khoja Shia mkoa wa Dodoma, Ustaadh Haidary Bakari, alisema anamuomba Mungu aiponye Tanzania na pia akaombea uchaguzi Mkuu ujao uwe wa heri na amani.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Maombezi wa Wanawake Barani Afrika, Prof, Margareth Kilimali, alisema anashukuru kwa kuwakutanisha viongozi hao wa dini wa mkoa wa Dodoma bila kujali tofauti zao za dini.

"Tunamshukuru Mungu kwa kuwa ana uwezo wa kutokomeza janga hili kwa nchi yetu Tanzania na bara zima la Afrika. Asante kwa fursa ya uchaguzi mkuu kwani umeshapanga ni jinsi gani utaendeshwa kwa amani wakati ukifika," alisema.

Maombi hayo maalum yaliandaliwa na TPA kwa kushirikiana na Bakwata, Shia, Hamadia, Hindu, Aga Khan, KKKT, EAGT, FPCT, Menonite na Morovian.

# Magufuli apongezwa msimamo corona

**Na Faustine Feliciane**

TAASISI ya Amani kwa Waislamu Tanzania (TIPF) imesema kauli ya hivi karibuni ya Rais John Magufuli juu ya janga la corona nchini ni ya kupongezwa na imejaa matumaini hususan katika matumizi ya dawa za kujifukiza.

Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Sadik Godigodi, alisema hayo jana huku akiwataka wataalamu wa kitaifa na kimataifa kuhakikisha wanafanyia kazi dawa hizo za asili zilizoonyesha matumaini katika kutibu ugonjwa huo.

"Kauli ya Rais wetu imetutia moyo sana. Awali kulikuwa na taarifa za kuogopa sana juu ya janga hili la corona. Sisi wananchi tuendelee kumwomba Mungu kama anavyotuasa Rais wetu lakini pia tuendelee kuchukua tahadhari ili ugonjwa huu usiendelee kusambaa na kuwa tishio kwetu," alisema Godigodi kwenye taarifa ya taasisi hiyo iliyotolewa jana.

Alisema Watanzania wazipuuze taarifa za mitandaoni ambazo hazina ukweli na zina lengo la kujenga hofu miongoni mwa wananchi.

"Lakini pia tufanyie kazi ushauri wa Rais Magufuli wa kuwa makini na misaada mbalimbali inayotolewa toka nje ya nchi kwa lengo la kupambana na corona. Baadhi ya misaada inaweza isiwe na nia njema kwetu kwani sasa dunia imebadilika sana," alisema Godigodi.

Alisema wataalam wa afya pia wanapaswa kufanyia kazi ushauri wa Rais Magufuli juu ya matumizi ya dawa hizo za hasili kama ilivyofanya Madagascar.

Kwa mujibu wa Godogodi, dawa inayoleta nafuu katika corona ni vyema ikafanyiwa kazi na wataalam wa afya katika kipindi hiki ambacho bado dawa sahihi haijapatikana.

"Lakini kwa sisi Waislam wakati tukiwa kwenye Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, tujitahidi sana kumwomba Mwenyezi Mungu atuepushe na janga hili la corona. Inshallah tutashinda vita hii huku tukijitahidi kufuata maelekezo ya wataalamu wetu," alisema Godigodi.

Pia alitaka wananchi kuwapuuza wanaobeza juhudi za Rais kwa kuwa vita hivi ni vikubwa ndiyo maana hata mataifa makubwa yameshindwa na kumwachia Mungu na kamwe Watanzania wasikubali kuyumbishwa na habari za mitandao ya kijamii.

Alisema Watazania wanatakiwa kusikiliza wataalamu wa afya pamoja na wasemaji rasmi walioteuliwa na serikali kuhusu janga hilo.

Sambamba na hilo, alimpongeza Rais kwa kutoliweka karantini jiji la Dar es Salaam kwa kuwa kama angefanya hivyo angesababisha taharuki kwa wananchi wa kawaida na kuyumbisha uchumi wa nchi.



Kiongozi wa Waislamu Shia Ithnasheriya Maulana, Sheikh Hemed Jalala (kulia), akiongea na waandishi wa habari kuhusu kuukaribisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, kwenye Masjid Ghadir Kigogo, jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Sheikh Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Shia Ithnasheriya Tanzania (TIC), Sheikh Abdallah Sefu. **PICHA:MIRAJI MSALA**

# Kesi kigogo Takukuru yapigwa kalenda

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imepiga kalenda kesi inayomkabili Mkurugenzi wa zamani wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathimini wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Kulthum Mansoor mpaka Mei 12, mwaka huu.

Kesi hiyo imepangwa kutajwa jana, lakini upande wa Jamhuri umedai mahakamani bado unaendelea na mazungumzo kati ya ndugu wa mshitakiwa huyo na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Ilitajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu,Thomas Simba, baada ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi, Godfrey Isaya anayesikiliza kesi hiyo kuwa na udhuru.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na kwamba bado upande wa Jamhuri unaendelea na mazungumzo na mshitakiwa kuhusu kukiri kosa.

Mshtakiwa huyo ambaye anakabiliwa na kesi ya Uhujumu Uchumi ikiwamo mashitaka manane ya kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanyanyifu na kutakatisha fedha kiasi cha bilioni 1.477, kuingia kwenye majadiliano na DPP, lakini wakashindwa kuelewana na majadiliano hayo yalikufa Januari, 2020 na baadaye mchakato ulianza upya.

Ilidaiwa katika tarehe tofauti kati ya Januari 2013 na Mei 2018, mshitakiwa alighushi barua ya ofa ya Agosti 13, 2003 kwa madhumuni ya kuonyesha kuwa, barua hiyo imetolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo huku akijua kuwa sio kweli.

Katika shitaka ya pili, inadaiwa kati ya Januari 2012 na Mei 2017 huko maeneo ya Upanga ndani ya Wilaya ya Ilala, mshitakiwa kwa udanganyifu alijipatia Sh. milioni 5.2 kutoka kwa Alex Mavika, ambaye ni mfanyakazi wa Takukuru kama malipo ya kiwanja kilichopo Kijiji cha Ukuni, Bagamoyo.

Pia inadaiwa kati ya tarehe hizo, Mansoor alijipatia Sh. milioni tatu kutoka kwa Wakati Katondo, kama malipo ya kiwanja kilichopo maeneo ya Kijiji cha Ukuni, wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani.

Mshtakiwa huyo pia alijipatia Sh. milioni tano kutoka kwa Ofisa wa Takukuru, Gogo Migutah, kama malipo ya kiwanja kilichopo eneo hilo hilo.




# BAYERN YAJIAMINI KUMBAKISHA NEUER

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich, inajiamini kwamba itaweza kumshawishi nahodha wake, Manuel Neuer kusaini mkataba mpya.

Golikipa huyo nyota alibainisha kukasirishwa na kuvuja kwa mazungumzo yake kuhusu mkataba mpya, ingawa hakuwa na taarifa za ndani zaidi kuhusu majadiliano hayo.

Raia huyo wa Ujerumani anataka kupewa mkataba mpya wa miaka mitano, huku akisema kwamba taarifa zilizovunja hazikuwa na ukweli wowote.

Katika mahojiano yake na gazeti la Bild wikendi iliyopita, Neuer alisema kwamba hakutendewa haki kuvujishwa kwa mazunguzo yake kuhusu mkataba mpya.

Lakini sasa Mkurugenzi wa Michezo wa Bayern, Hasan Salihamidzic, anaamini kwamba watafikia makubaliano na golikipa huyo.

"Tulishatolea ufafanuzi wa ndani kuhusu yale yaliyojitokeza," alisema Salihamidzic. "Na tangu wakati huo mambo yanakwenda vizuri sana na kila kitu kipo sawa."

"Manuel anajua kwamba tunamheshimu sana," aliongeza Salihamidzic na kusema; "Nimecheza na Oliver Kahn. Najua kiwango chake kilivyo, hivyo Manuel ni golkipa wa kiwango cha juu kabisa, natumaini ataongeza mkataba wa kucheza hapa."

# De Gea ataka kuzeekea Man United

**MANCHESTER,** England

DAVID de Gea ameelezea kukaa kwake karibia muongo mmoja pale Manchester United ni kama "ndoto" na ana mpango wa kubakia hapo Old Trafford kwa muda mrefu zaidi.

De Gea mwenye umri wa miaka 29, alijiunga na United akitokea Atletico Madrid mwaka 2011 kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 19, ambayo ilikuwa rekodi kwa Uingereza kwa kipa kunUnuliwa kwa kiasi hicho cha fedha.

Baada ya kukaa hapo kwa muda mrefu, De Gea amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa makipa bora duniani kwa sasa.

Uhamisho wa kwenda Real Madrid ulishindikana Agosti mwaka 2015, lakini raia huyo wa Hispania alisaini mkataba mpya na baadaye alikubali kuongeza muda Septemba mwaka jana, ambapo sasa atakaa hapo hadi mwaka 2023.

Lakini kiwango cha De Gea kwa miaka michache iliyopita hakijawa cha kuvutia kama wengi walivyomtarajia, huku mashabiki wa United wakimtaja Dean Henderson arudi kubeba jahazi–ambapo kwa sasa anacheza kwa mkopo kule Sheffield United.

"Kuwa tu sehemu ya klabu hii ni jambo la kuvutia. Fikiria karibia miaka 10 nimekuwa hapa, hii ni kama ndoto," alisema De Gea akinukuliwa na tovuti ya klabu hiyo.

"Ni jambo zuri kucheza katika klabu hii, hivyo natumaini nitakuwa hapa kwa miaka mingi, miaka mingi sana."







# *Giroud kufungwa upya Chelsea*

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Olivier Giroud, anatarajia kusaini mkataba mpya wa mwaka mmoja ambao utamuweka klabuni hapo hadi mwaka 2021.

Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 33, alionekana kama angeondoka Januari baada ya kucheza mechi tatu za Ligi Kuu wakati akiingia kwenye miezi yake sita ya mwisho kwenye mkataba wake.

Alikuwa akihusishwa na mpango wa kubakia Inter Milan, lakini baada ya kuumia kwa mshambuliaji mwenzake, Tammy Abraham, Januari, Giroud alionyesha kiwango cha kuvutia kwa kufunga mabao mawili kwenye mechi nne za Ligi Kuu.

Kocha, Frank Lampard, alisifia morali ya mshambuliaji huyo wa zamani wa Arsenal mwishoni mwa dirisha dogo la Januari, licha ya kutokuwa chaguo la kwanza.

Alisema: "Olivier Giroud ameonyesha kiwango cha kuvutia katika kipindi hiki na anaonekana ni mtu anayejielezea vizuri zaidi."

Giroud aliondoka Arsenal na kujiunga na Chelsea Januari mwaka 2018 kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 18 awali akitua kwa mkopo wa miezi 18. Kisha Mfaransa huyo akaongeza mkataba wake kwa mwaka mmoja Mei, mwaka jana.

# Newcastle yajitosa usajili wa Koulibaly

**NEWCASTLE,** England

KLABU ya Newcastle United ambayo kwa sasa ipo sokoni na inakaribia kuuzwa kwa kampuni ya kutoka Saudi Aarabia, imepanga kuzungumza na Napoli kuhusu usajili wa mlinzi wa kati, Kalidou Koulibaly.

Newcastle sasa inajipanga kukisuka upya kikosi chake na tayari imeanza kunyemelea saini za wachezaji nyota Ulaya.

Mshambuliaji nguli wa Paris Saint Germain (PSG) Edinson Cavani na Nabil Fekir wapo katika rada za klabu hiyo ya St James Park.

Koulibaly amekuwa akihusishwa na Manchester United ambayo inapewa nafasi baada ya Napoli kumuweka sokoni.

Mmiliki wa Napoli Aurelio De Laurentiis yuko tayari kumpiga bei beki huyo wa kimataifa wa Senegal.

Newcastle ambayo kwa muda mrefu imekuwa katika mazingira magumu ya kiuchumi, imetuma maombi ya usajili wa beki huyo wa kati pia Cavani na Fekir.







# KLOPP AMPIGIA SIMU BABA WA MBAPPE

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp ameripotiwa kumpigia simu baba mzazi wa mshambuliaji wa PSG, Kylian Mbappe, ili amshawishi nyota huyo kujiunga na Liverpool kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Mbappe ambaye kwa sasa anatajwa kama mmoja wa wachezaji wenye thamani kubwa zaidi duniani, klabu kadhaa zimetajwa kuiwania saini yake ikiwamo Real Madrid ya Hispania.

Mbappe anatajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 250 kwa klabu yoyote itakayotaka kumsajili, ingawa PSG wenyewe wanaweka ngumu kumuuza.

Hata hivyo, inaelezwa Klopp naye kaingia kwenye vita ya kumsaka Mbappe wakati akijiandaa kumpoteza Sadio Mane anayewindwa pia na Real Madrid.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka nchini Ufaransa ni kwamba, Klopp amewasiliana na baba wa Mbappe ili amshawishi aweze kujiunga nao katika dirisha lijalo la majira ya kiangazi.

Taarifa zinasema kuwa Klopp anajaribu kuingilia vita hii juu kwa juu kwa kutumia njia mbadala ili kufanikiwa kuinyakuwa saini ya mchezaji huyo ambaye alikuwa karibu zaidi kujiunga na Real Madrid kabla ligi haijasimamishwa kutokana na hofu ha maambukizo ya virusi vya corona.

Mbappe msimu huu amefunga mabao 30, katika michuano yote akiwa na klabu ya PSG, huku Liverpool wao wakiwa kwenye uongozi wa msimamo wa Ligi Kuu nchini England wakiwa na tofauti ya pointi 25.

Mchezaji huyo alikuwa anahusiswa na klabu nyingi kabla ya kujiunga na PSG kutokea klabu ya Monaco.

Huku taarifa kutoka nchini Hispania zikidai kwamba Klopp atakumbana na upinzani mkubwa kutoka kwa wakala wa Mbappe ambaye aliwahi kucheza na kocha wa Real Madrid, Zinadine Zinade, lakini pia akiwa ni rafiki mkubwa wa kocha huyo.

# *Pogba kugeuzwa chambo ya Sancho*

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imebainisha kwamba, iko tayari kumuuza kiungo wake, Paul Pogba ili kupata fedha za kumsajili Jadon Sancho.

Man United ipo kwenye harakati za kutaka kumsajili Sancho ambaye anacheza kule Borussia Dortmund wakati wa dirisha la majira ya joto. Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, Man United sasa wanataka kumuuza Pogba ili kupata pauni milioni 100 za kumnunulia Sancho kutoka Dortmund.

Uamuzi huo umefikiwa baada ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa Man United, Ed Woodward kudai klabu hiyo haitatumia fedha nyingi katika usajili wa msimu ujao.

Wachezaji wengine wanaotarajiwa kuwekwa sokoni ni Jesse Lingard, Marcos Rojo na Andreas Pereira.

Woodward ameonya hana bajeti ya usajili pana kutokana na mtikisiko wa kiuchumi uliosababishwa na janga la maambukizo ya virusi vya corona (covid-19).



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BABA AUBAMEYANG AMBAKISHA EMIRATES

## Lakini Arsenal yakatisha mazungumzo, United, Inter na Barca zajitosa huku...

**LONDON,** England

ARSENAL imeripotiwa kufunga mazungumzo ya mkataba mpya na mshambuliaji wao Mgabon Pierre-Emerick Aubameyang - licha ya baba wa mchezaji huyo kusema kwamba anapaswa kusaini mkataba mpya.

**Aubameyang amekuwa akihusishwa na kuondoka Emirates majira haya ya joto, huku Manchester United, Inter Milan, Barcelona, Real Madrid na Chelsea zote zikiaminika kuvutiwa kupata saini yake.**

Straika huyo wa 'Gunners' na Jamie Vardy wa Leicester City ni washambuliaji wawili pekee katika Ligi Kuu England waliopo kileleni mwa orodha ya wafungaji bora kila mmoja akiwa na mabao 17 msimu huu, na sasa anaingia mwaka wake wa mwisho kwenye mkataba wake na Arsenal inazingatia kwamba inaweza kumpoteza bure mwishoni mwa msimu ujao.

Mazungumzo yamekuwa yakiendelea kuhusu mkataba mpya, lakini mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 30, inaaminika anataka kuboreshewa mshahara wake wa sasa wa pauni 200,000 kwa wiki- jambo ambalo linaweza kuthibitishwa kuwa gumu kwa sababu ya kurudishwa nyuma kifedha kutokana na kuibuka kwa janga la virusi vya corona.

Na sasa Arsenal imeweka kando mazungumzo hayo, kwa mujibu wa gazeti la The Express - na Inter Milan ikiripotiwa kuongoza katika mbio za kumsajili majira ya joto.

Gazeti hilo limeeleza Kocha wa 'Nerazzurri' hao, Antonio Conte yupo tayari kumpeleka Aubameyang Milan, na nyota huyo wa kimataifa wa Gabon ameripotiwa kuwa tayari kusikiliza ofa itakayotoa Inter.

Hii ni licha ya baba wa mchezaji huyo kumtaka mtoto wake kusaini mkataba mpya hapo Emirates kwa kutoa wazo kubwa katika mtandao wa kijamii.

Katika ujumbe wake kupitia akaunti yake ya Instagram, Pierre-Francois Aubameyang aliposti picha ya mwanawe akisaini mkataba wake wa kwanza na Arsenal mwaka 2018, ikiambatana na maelezo: "Unajua nini cha kufanya bro @aubameyang97."

Arsenal wapo tayari kushusha gharama zao za mishahara chini, lakini inajua wanakabiliwa na ugumu kwa kuzingatia mchezaji anayelipwa kiasi kikubwa na klabu, Mesut Ozil, anayepokea pauni 350,000 kwa wiki katika mkataba wake.

## ZISIKUPITE

### NEYMAR CHUPUCHUPU CHELSEA

CHELSEA ilikaribia kumsajili Neymar miaka mitatu iliyopita kabla ya kuondoka Santos na kujiunga na Barcelona, kwa mujibu wa mmoja wa mawakala wa zamani wa nyota huyo wa PSG. ***(The Sun)***

### JUVE YAMTAKA ALBERTO

LIVERPOOL ipo karibu kujiimarisha kifedha kutokana na Juventus kutaka kumsajili Luis Alberto, ambaye miamba hiyo ya Anfield imejumuisha asilimia 30 ya ada ya mauzo wakati ikimnunua kutoka Lazio mwaka 2016. ***(Daily Express)***

### SAKA AWAFIKIRISHA ARSENAL

BUKAYO Saka amewaacha mashabiki wa Arsenal wakikuna vichwa wakati aliposti video ya kijinga katika mtandao wa kijamii huku beki huyo wa kushoto akihusishwa na kujiunga na Borussia Dortmund. ***(Daily Mirror)***

### NDIDI AJIBAKISHA LEICESTER

WILFRIED Ndidi amejiweka mbali mwenyewe kuhusu uwezekano wa kuondoka Leicester City kwa kukiri hana sababu ya kuondoka katika klabu hiyo. ***(Daily Mail)***

### CITY KUMFUATA BONUCCI

MANCHESTER City ipo tayari kuiimarisha safu yake ya ulinzi kwa kumsajili beki wa kati wa Juventus, Leonardo Bonucci ***(The Sun)***

### ATAKIWA NEWCASTLE

NEWCASTLE imefungua meza ya mazungumzo na beki wa Napoli, Kalidou Koulibaly na pia inataka kumsajili mshambuliaji wa PSG, Edinson Cavani na wa Real Betis, Nabil Fekir ***(Daily Express)***

### ARSENAL YAMUWINDA WILLIAN

ARSENAL tayari imeripotiwa kupiga hatua zaidi ya Liverpool katika mbio za kumsajili winga wa Chelsea, Willian kwa ada huru majira haya ya joto. ***(Daily Mirror)***

### LIVER YAMKATAA COUTINHO

KIUNGO wa Barcelona, Philippe Coutinho, ambaye yupo Bayern Munich kwa mkopo, ameambiwa na Liverpool kuwa haivutiwi kusajili tena wakati nyota huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 27 alipojadili uwezekano wa kurudi Anfield. ***(Mirror)***

### DE GEA KUZEEKEA UTD

KIPA wa Manchester United, Mhispania David de Gea, amesema anataka kubaki Old Trafford kwa "miaka mingi" lakini mlinda mlango huyo mwenye umri wa miaka 29, anakabiliwa na ushindani katika nafasi hiyo kutoka kwa Muingereza Dean Henderson, 23, ambaye amevutia akiwa kwa mkopo Sheffield United. ***(Mail)***

### MEUNIER SAFI KWA MOURINHO

BEKI wa Paris St-Germain na Ubelgiji Thomas Meunier amekuwa "akishinda dhidi" ya kocha wa Tottenham, Jose Mourinho kuelekea dirisha la usajili la majira ya joto, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, bado ana matumaini ya kupewa mkataba mpya hapo Parc des Princes. ***(L'Equipe, via Teamtalk)***

HABARI MICHEZO

# Matola: Ni ngumu kufuatilia mazoezi

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, kueleza kwamba ametoa programu maalumu kwa kila mchezaji wakati huu wakiwa mapumzikoni kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19), msaidizi wake, Selemani Matola, amesema ni ngumu kwa sasa kufuatilia maendeleo ya wachezaji iwapo wanafanya mazoezi au la wakiwa nyumbani.

Machi 17, mwaka huu serikali ilitangaza kusimamishwa kwa shuguli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwamo michezo kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, hivyo makocha wengi wakaingia katika mpango wa kuandaa programu za mazoezi binafsi kwa wachezaji wao.

Lakini Matola amemwambia mwandishi wetu kuwa ni vigumu sana kuwafuatilia wachezaji wa Bongo kutokana na mazingira yaliyopo.

"Kuwafuatilia wachezaji wakiwa nyumbani ni vigumu kutokana na mazingira yaliyopo hasa kwetu Bongo, tunaelewa namna mambo yalivyo.

"Hiyo haina maana kwamba kwa kuwa hakuna namna ya kuwafuatilia basi wasifanye mazoezi haitakuwa sawa, wanapaswa kufanya mazoezi na kuchukua tahadhari ya ugonjwa huu," alisema.

# Malale ataka straika, winga

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Hamsini Malale, amesema anahitaji mshambuliaji na winga mmoja katika usajili wake kwa lengo la kuboresha kikosi chake kwa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Malale alisema upungufu aliouona katika kikosi chake ni katika nafasi hizo mbili na tayari wameshawaona nyota hao wanaowahitaji lakini ni mapema sana kuweka wazi kwa sasa kabla ya kumalizana nao.

"Kikosi changu kipo vizuri, ila kuna upungufu ambao nimeuona na kufanyia kazi katika usajili wetu ujao, ambapo tutapaswa kuongeza mshambuliaji mmoja na winga, tayari wapo na muda ukifika tutaweka wazi," alisema Malale.

Alisema ni mapema kutaja majina ya wachezaji hao kutokana na kuwa bado wapo katika majukumu ya timu zao huku dirisha la usajili likiwa bado halijafunguliwa.

"Hao wachezaji wanatoka katika timu zetu za chini, sitarajii kuingia huko katika klabu kongwe na kubwa katika usajili wetu kwa sababu nina imani na nyota kutoka chini kufanya vizuri na kufikia malengo yangu," alisema Malale.

# MORRISON AWATAKA YANGA KUSALI JANGA CORONA LIPITE

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU chache baada ya nahodha msaidizi wa Yanga, Juma Abdul, kueleza amekumbuka manjonjo ya mshambuliaji wao, Bernard Morrison, hatimaye Mghana huyo ameibuka na kuwataka Wanayanga wote kusali ili ligi hiyo irejee waweze kufurahia soka.

Ligi Kuu imesimama kwa kipindi kisichojulikana kutokana na agizo la serikali ili kuepuka maambukizo ya virusi vya corona ambavyo vinaitesa dunia kwa sasa kutokana na watu wengi kupoteza maisha duniani kote.

Morrison ambaye alisajiliwa katika dirisha dogo la msimu huu, amekuwa kivutio si tu kwa wachezaji wenzake bali mashabiki wa timu hiyo na jana aliwataka mashabiki kuendelea kumuomba Mungu janga hili la corona lipite.

**"Tuendelee kumuomba Mungu maisha ya kawaida yarejee baada ya hili janga la corona na turudi kufanya kazi ili mashabiki na wapenda soka wafurahie kazi yetu," alisema Morrisson ambaye amekuwa kivutio kwa mashabiki wa Yanga**

Morrison alisema kwa sasa anaendelea kuchukua tahadhari akiwa nyumbani na kuwataka mashabiki wa timu hiyo nao kufanya hivyo ili kujiepusha na janga la corona.

Wiki iliyopita nahodha msaidizi wa Yanga, Abdul, alisema kwa sasa wamekuwa wanyonge nyumbani kutokana na kushindwa kuendelea kupambana kwenye Ligi Kuu Bara jambo linalomfanya kukumbuka manjonjo ya Morrison.

"Mambo ni mengi ambayo nimekumbuka ndani ya ligi ikiwa ni pamoja na vitu vya Morrison uwanjani ukiachana na hayo pia namna mashabiki ambavyo walikuwa wanatupa sapoti ilikuwa ni raha," alisema Abdul.

'KI-BARAKOA'...



Kiungo wa Simba, Mkenya Francis Kahata, akifanya mazoezi peke yake kwao jijini Nairobi, huku akiwa amevalia barakoa, katika kipindi hiki timu yake ikiwa imesitisha mazoezi ya pamoja kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona (COVID-19). **PICHA: MTANDAO**

# *Miembeni waitaka ZFF kufuta Ligi Zanzibar*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HUKU ikionekana kupoteza nafasi ya kupanda Ligi Kuu msimu ujao, timu ya Miembeni inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, imesema haioni haja msimu huu kuendelea, hivyo ni bora Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), likakaa chini na kuangalia namna ya kumaliza msimu au kuufuta kabisa.

Kama ilivyo kwa Ligi Kuu Zanzibar, pia Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja kwa sasa imesimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19), na hadi inasimama Miembeni ipo nafasi ya 12 ikiwa na alama 14 baada ya kushuka dimbani mara 17 kwenye ligi hiyo inayoshirikisha timu 13.

Akizungumza na gazeti hili Mwenyekiti Msaidizi wa timu hiyo, Mbarouk Abdallah Hanga alisema kwa sasa wachezaji wamekaa muda mrefu pasipo kufanya mazoezi ya pamoja, hivyo hata ligi hiyo ikiendelea lazima ZFF iangalie njia na mbinu ambayo haitaathiri timu na wachezaji kwa ujumla.

Alisema hawezi kutilia mkazo sana njia ya kufutwa kwa ligi kama inavyosemwa na baadhi ya wadau wa soka kutokana na suala hilo uamuzi wake unahitaji ushirikishwaji wa hali ya juu pamoja na makubaliano ambayo klabu zitaridhia.

"ZFF iangalie kwa umakini kuhusu msimu huu, kwa mtazamo wangu bora ligi hii ifutwe maana hata tukisema tusubiri huu ugonjwa umalizike kwa mujibu wa taratibu na misimu ya ligi inavyokwenda tutakuwa nje ya muda.

"Kama ikishindikana kufutwa basi shirikisho watoe uamuzi ambao hautakuja kuleta athari kwa timu au wadau wa soka wanaofuatilia timu zao, na uamuzi wowote utakaotolewa basi ni vema kushirikisha pande zote ili kuepuka lawama hapo baadaye,"alisema.

Aidha, alisema kipindi hiki kilikuwa cha kufanya usajili kwa ajili ya msimu mpya wa 2020/21, hivyo kutokana na kuwapo kwa ugonjwa huo wa Covid-19, ligi zote zimeshindwa kumalizika kwa wakati, na kwamba kumeleta athari kwa klabu ambazo zimetumia gharama kubwa kuhudumia timu hasa ikizingatiwa klabu nyingi za Zanzibar ni masikini.

Michezo
Jumanne Aprili 28, 2020
Nipashe



Baba Aubameyang ambakisha Emirates

UKURASA 22

HUYU HAPA...



Kiungo Ally Niyonzima (kushoto) anayewindwa na Yanga, akiwa mazoezini. **PICHA: MTANDAO**

## Wawa na mazito ya Ligi Kuu Simba

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI hatima ya kurejea kwa Ligi Kuu Bara ikiwa bado haijulikani, wachezaji wameanza kueleza namna wanavyoikosa ligi hiyo pamoja na mambo mengine yanayowapa furaha dimbani.

Ligi Kuu imesimama kwa kipindi kisichojulikana kutokana na agizo la serikali la Machi 17, mwaka huu la kusitisha shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwamo michezo ili kuepuka maambukizo ya virusi vya corona vinavyoitesa dunia kwa sasa na kusababisha maelfu ya vifo duniani kote. Na ikiwa ni mwezi mmoja na takriban wiki mbili tangu ligi hiyo isimame, beki wa kati wa Simba, Muivory Coast Pascal Wawa amekumbuka mengi katika ligi hiyo.

"Nakumbuka mambo mengi, nakumbuka michezo ya VPL, nawakumbuka wachezaji wenzangu na pia nawakumbuka mashabiki wetu ambao huwa wanakuja kutushangilia," alisema Wawa jijini Dar es Salaam jana.

Aidha, Wawa kupitia mtandao wa klabu hiyo, alitaka kujua mashabiki wao wanakumbuka nini katika ligi hiyo akihoji "Wewe unakumbuka nini baada ya michezo yote kusimama".

Kadhalika, winga mshambuliaji wa Yanga, Mghana Bernard Morisson, jana aliwataka mashabiki wa timu hiyo kuendelea kuomba ili ligi hiyo irejee waendelee kufurahia mambo mazuri kutoka kwao.

# Kumekucha usajili Yanga

## Corona yaichelewesha GSM kwenda kumaliza biashara ya Ally Niyonzima, yaelezwa...

**Na Saada Akida**

LICHA ya wiki iliyopita Makamu Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga, Fredrick Mwakalebela, kueleza kuwa sasa wanaendesha mchakato wao wa usajili kimya kimya ili kukwepa hujuma kutoka kwa klabu zingine za Ligi Kuu Bara, Nipashe limebaini tayari safari ya kiungo kutoka Rayon Sports ya Rwanda, Ally Niyonzima inanukia Jangwani.

**Kwa muda mrefu Yanga imekuwa ikielezwa kuwa katika mchakato wa kuipata saini ya kiungo huyo kabla ya wiki iliyopita, Mwakalebela alieleza kwamba kwa sasa kila kitu katika klabu hiyo ni "kimya kimya" hadi watakapomalizana na mchezaji wanayemtaka.**

Lakini taarifa za uhakika zilizolifikia Nipashe jijini Dar es Salaam jana kutoka kwa chanzo chetu cha uhakika ndani ya klabu hiyo, ambacho hakikuwa tayari kutajwa jina lake, kilieleza kuwa suala la nyota huyo limekabidhiwa kwa Kocha Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael, ambaye tayari alishabisha hodi Rayon Sports na kuelezwa dau la kumpata kiungo mkabaji huyo.

Chanzo hicho kilieleza, Eymael alisharejesha mrejesho kwa uongozi wa Yanga na kwamba kila kitu kipo mezani mwa mdhamini mkuu wa klabu hiyo, Kampuni ya GSM, ambayo inasubiri kumalizika kwa karantini ya corona nchini Rwanda ili kwenda kumaliza biashara.

"Mchezaji ambaye kocha anavutiwa naye ni huyo na yeye mwenyewe amekubali kubeba jukumu na kufanya makubaliano na klabu na wawakilishi wake, kila kitu ametekeleza, tunasubiri muda ukifika sula hilo litawekwa wazi," kilieleza chanzo hicho.

Hivi karibuni Eymael aliwahi kuliambia gazeti hili kwamba, tayari ameanza kufanya mazungumzo na kiungo mkabaji mmoja kwa ajili ya kupata saini yake, lakini sasa imebainika ni Ally Niyonzima.

Alisema amepanga kushusha kiungo mmoja mkabaji wa kimataifa atakayecheza namba sita baada ya kugundua upungufu katika safu hiyo.

Kocha huyo hakuwa tayari kutaja jina la kiungo anayemhitaji, kabla ya juhudi ya Nipashe jana kugundua Mnyarwanda huyo mwenye kimo cha mita 1.87 huku akitumia mguu wa kulia.

Niyonzima mwenye umri wa miaka 24, ambaye pia aliwahi kuichezea Sofapaka ya Kenya, alitua Royon Sports ya kwao Rwanda kwa uhamisho huru akitokea Al Bashaer SC ya Oman Januari 15, mwaka huu.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042